


ISHARA KUU

 Na tuombe. Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe, usiku wa leo, kwamba Wewe ungali ni yule MIMI NIKO mkuu, si yule “Nilikuwa” au “nitakuwa.” Wewe ni wakati uliopo, Mungu wetu. Na Wewe ni yule yule leo, jana, na hata milele, Mungu asiyebadilika. Tunakushukuru Wewe kwa sababu kwamba tuna majaliwa haya ya kujua hili, ambalo limefunuliwa kwetu na Roho Mtakatifu. Pia Yeye ametutia muhuri ndani ya Ufalme wa Mungu, pamoja na Yeye, kwa ile Ishara ambayo Yeye alituachia. Tunashukuru sana kwa Hiyo. Tubariki, usiku wa leo, tunapokungojea Wewe. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

Mwaweza kuketi.

2 Inanibidi, kuweka tu chache za lesa hizi hapa pembeni, ninii tu...Tunaenda kuwaombea wagonjwa, kwa siku zilizosalia usiku, Bwana akipenda. Tunaenda kufanya hivyo. Hata hivyo, nilimwambia Billy kwamba alikuwa amechelewa kidogo, usiku wa leo, na hakuweza kusambaza kadi za maombi, lakini hata hivyo tulifikiria labda huenda tukafanya hivyo wakati nilipokuwa labda nafanya wito wa madhabahuni, au kitu fulani, tungeweza kufanya hivyo.

3 Sasa kila mtu anahisi vyema? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hilo ni sawa. Ha—hakika nina furaha kusikia hilo.

4 Sasa, ninaamini imetangazwa kwamba kiamshakinywa cha Wafanyabiashara ni asubuhi. Ninaamini kwamba wao, ni, wameshatangaza wakati, na kadhalika. Sasa hebu tuwe tayari kwa chochote kile Bwana angetutaka tufanye. Tunatambua kwamba huu ndio usiku ambao chochote chaweza kutokea, kwa hiyo tunataka kuwa tayari kwa hicho, na upesi tuingie katika Ujumbe. Kwa hiyo, kesho tuna siku yenye shughuli nyingi kwelikweli.

5 Ndipo Jumapili, kama Jumapili asubuhi, nafikiri ninapaswa kuzungumza hapa baada ya shule ya Jumapili, Jumapili asubuhi; na Jumapili usiku. Kwa hiyo, mmealikwa kwenye mikutano hii yote. Ikiwa, bila shaka, kama una mahali pa wajibu mahali fulani, kwamba inakupasa kuwa huko, vema, tusingetaka ukose hiyo.

6 Nina arusi, wakati fulani, ama kesho au siku inayofuata. Jumapili asubuhi, naam, inanibidi kuoza mume na mke kutoka maskani yangu. Na kwa hiyo tunatarajia kuona hii pia.

7 Na sasa mtuombe tunapojitahidi kusoma baadhi ya Neno la Mungu sasa hivi, na kuingia moja kwa moja katika Ujumbe, upesi. Walinitaka nije mapema kwa sababu ya umati

unaosimama. Na kwa hiyo tutasoma kutoka Isaya, mlango wa 7. Ninataka kusoma, kuanzia kwenye kifungu cha 10.

Tena BWANA akasema . . . na Ahazi akinena,

Jitakie ishara ya BWANA, Mungu wako; itake katika mahali palipo chini sana, au mahali palipo juu sana.

Lakini Ahazi akasema, Sitaitaka, wala sitamjaribu BWANA.

Naye akasema, Sikilizeni sasa . . . enyi nyumba ya Daudi; Ni neno dogo kweni kuwachosha wanadamu, lakini je! mnataka kumchosha Mungu wangu pia?

Kwa hiyo BWANA mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.

8 Kama ningeliita hili kwa ajili ya somo, usiku wa leo, kuzungumzia kwa dakika chache, juu ya muhtasari fulani ambao nimeandika alasiri ya leo hapa, ningependa kuzungumza juu ya . . . kuchukua somo la, *Ishara Kuu*.

9 Mnajua, hii ni siku kuu, kila kitu ni kikuu. Na sisi tunaona kwamba ra—radi iliyogawanyika angani kwenye usiku wenye mawingu, hakika hututangazia kwamba kunaweza kuwa na nuru katika giza. Tunajua hilo.

10 Mungu alijua mwisho tangu mwanzo, hivyo basi Yeye angeweza kupanga kila kitu, kwamba ingeweza tu kufanya kazi kwa utukufu Wake. Na hiyo inatupatia ujasiri, kujua kwamba haijalishi ni nini kinachotukia, Mungu anafanya kila kitu, saa inapiga tu kwenye wakati hasa.

11 Wakati mwingine tunakuwa wachovu, tumevurugika. Tunakuwa na pupa. Tunawazia, “Loo, lazima tufanye *hili*, au tufanye *lile*.”

12 Lakini, kumbuka, saa ya Mungu itakuwa tu kwenye wakati hasa. Mambo haya yote hayana budi kuwa hivi. Yote hayana budi kufanywa kulingana na maarifa Yake makuu, kujua Kwake kimbele, kwani kwa kujua kimbele Yeye aliweza kuchagua kimbele, si kwa shauku Yake, bali kwa kujua Kwake kimbele. Mungu hachagui kimbele kwa shauku Yake. Yeye hataki mtu yeyote aangamie, lakini kwa kujua Kwake kimbele Yeye alijua ni nani angelikubali na ni nani asingekubali. Hivyo basi Yeye anaweza kufanya kila kitu kifanye kazi kulingana na saa Yake kubwa inayopigapiga, kwa kuwa Yeye angeweza kutaja kimbele mwisho tangu mwanzo. Na, kwa hiyo, Yeye alijua kwamba sisi tungeishi katika siku hii. Alijua kwamba hii ingekuwa ni siku yetu. Alikuwa na mipango kwa ajili ya siku hii. Amekuwa na mipango kwa ajili ya kila siku. Na kamwe hata mpango Wake mmoja haujawahi kushindwa. Yeye daima huwa kwenye wakati ufaao.

¹³ Na huu ndio ambao tunaita wakati mkuu. Kila kitu unachoonna siku hizi lazima kiwe “kikuu,” la sivyo hakitapita, kama huna kitu kikuu, kwa sababu ni wakati mkuu. Wamekuwa na wakati wao, na wamekuwa na, sasa wanao wakati mkuu, kila kitu tuonacho.

¹⁴ Huwezi kushuka chini kwenye duka la uchochoroni tena, na kupata pande kubwa la jibini limewekwa hapo kama ulivyozoea kupata. Na—na jinsi ilivyokuwa, maskini maduka ya uchochoroni, kama ulikuwa hata na chakula kizuri sana, kila mtu anataka kwenda kwenye duka lililo bora zaidi, lililoyozwa, linaloitwa duka kubwa. Hawana budi kwenda hapo hata kama wanalipa zaidi kwa ajili ya chakula chao. Inawabidi kwenda kwenye duka kubwa. Hiyo ni kweli. Kwa sababu ni kubwa. Unaona? Kila mtu anataka kitu fulani kikuu.

¹⁵ Na, leo hii, huwezi kuchukua motokaa ya kawaida. Muundo wa kale wa T ungekanyagwa, huko nje barabarani sasa. Wana motokaa kubwa. Inabidi Ford kuwatengenezea iliyo kuu. Chevy lazima iwatengenezee iliyo kuu. Wengine wote, wakitarajia kuendelea katika mashindano, inawabidi kuwatengenezea iliyo kuu. Kila kitu ni kikuu, kikuu, kikuu.

¹⁶ Baada ya kitambo, tunafikia wakati wa anga. Sasa walikuwa na ndege ya rafadha. Halafu, muda si muda wajua, wakaja na jeti. Na sasa wanayo jeti kuu. Unaona, inabidi iwe kuu. Kama sivyo, haiko—haiko kwenye wakati unaofaa. Kila kitu katika wakati huu hakina budi kuwa kikuu.

¹⁷ Tulikuwa na barabara za kale tulizokuwa tukisafiri, sasa mna barabara kuu. Inabidi iwe na vijia vinne au vitano vinavyoelekea upande mmoja, na vijia vinne au vitano vinavyokuja upande mwingine, la sivyo utakanyagwa. Unaona? Inakubidi kuwa navyo, maana huu ni wakati mkuu, majira makuu. Kila kitu kiko katika ukuu.

¹⁸ Hata tunadhania kwamba tuna watu wakuu, ama watu fulani wanadhania kwamba wao ni wakuu, na wanajaribu kutenda hivyo, kwa vyovyote vile. Jamii iliyo kuu, jamii moja ikitaka kutawala nyingine.

¹⁹ Makanisa makuu, madhehebu makuu, kila kitu kinakuwa kikuu. “Kama si kikuu, vema, sivyo.”

²⁰ Nafikiri hata wanawake wanakuwa na mavazi makuu, wakati wa kisasa. Viatu vya mtindo wa kale, vilikuwa na ngozi ndani yake, unavinunua yapata dola tatu kwa jozi, aina bora kuliko zote, ilikuwa na ngozi zaidi ndani yake kuliko jozi dazani moja zilizo nayo leo hii, ambazo unalipia dola ishirini na tano. Lakini inabidi iwe aina kuu, mwajua, visigino karibu *hivyo*, na hakina vidole, lakini ni kikuu. Unaona, ndilo jambo. Karibu inakubidi kuwa katika mapindo makuu ili kutembea navyo, unaona. Hiyo ni kweli. Kila kitu kimeingia kichaa, kwangu mimi, unaona. Lakini ni—ni wakati mkuu. Ni majira makuu.

²¹ Dalili hizi zote ni—ni alama ya giza la kiroho. Mambo haya yote ambayo tunaona yakitendeka katika haya makuu, makuu, makuu, laiti tu tungalijua! Tuko mbioni, inatubidi kufika kule, na tunafanya nini tukifika kule? Ilikuwa inachukua, kutembea kwenda nyumbani kutoka kazini, ilikuwa kwamba watoto iliwabidi kutembea kwenda shuleni, na sasa wanalo basi linalokuja mlangoni kuwachukua na kuwapeleka hadi shuleni na wakitoka shuleni, na halafu wanalipa dola nusu milioni kwa ajili ya chumba cha burudani, kuwapa zoezi kidogo, la sivyo wanakufa. Vema, walikuwa wanalipata hilo wakitembea kwenda shuleni. Wakati mkuu! Sasa si hiyo ni kweli? Hata makanisa inawabidi kuwa na, hawana shughuli za kutosha miongoni mwao, inawabidi kuwa na chu—chu—chumba ambamo wote wanaweza kucheza na kuruka juu-chini. Ilikuwa kwamba Roho aliwafanya kufanya hivyo, lakini sasa inawabidi kuenda huko nje, namna fulani ya majira makuu. Unaona, yote yakieleleza kwenye giza la kiroho, siku mashuhuri tunayoishi.

²² Mnajua, watu Wake, watu wa Mungu wa Biblia, daima wameonywa, na Mungu, kuzitazama ishara za wakati. Yesu, wakati Yeye alipokuwa duniani, aliwaambia Mafarisayo wa siku Yake, Yeye akasema, “Enyi Mafarisayo vipofu.” Kasema, “Mnatoka nje wakati wa jioni na mnaangalia na kuona anga zimetanda na ni nyekundu,” kasema, “‘Kesho,’ mtasema, ‘kutakuwa siku angavu.’” Ndipo Yeye akasema, “Ndipo mnatoka nje nayo ni mazito, yanaonekana yenye hasira, basi, ‘Kesho hali ya anga itachafuka.’” Akasema, “Mwaweza kupambanua uso wa anga, bali ishara ya wakati hamwezi kupambanua.” Kasema, “Kama mngalinijua Mimi, mngalijua siku Yangu. Kama mngalimjua Musa,” Yeye akasema, “mngalinijua Mimi, kwa sababu Musa aliandika habari Zangu.”

²³ Kwa njia nyingine, kama ambavyo nimekuwa nikisema, wangelijua kwamba Maandiko ambayo hayana budi kutimizwa katika siku hiyo yalikuwa yanatimia, na wao hawakujua hilo. Walikaza ma—macho yao sana juu ya mapokeo yao, na kadhalika, mpaka hawangeweza kuona Maandiko yenyewe yakijifunua mbele zao.

²⁴ Ningefananisha wakati huu na ule. Kwamba hata miongoni mwa wa—watu wazuri, wakati mwingine, wanakosa kuliona. Wanaondoka tu na kwenda, na, kwa uaminifu, ni—ni... Ingenishusha moyo kama nisingejua kwamba Yesu alisema kile Yeye alichosema juu yake, kwamba, “Hakuna mtu awezaye kuja isipokuwa Baba Yangu amvute, na wote Baba alionipa Mimi watakuja.” Kamwe hawataweza kuona Hilo. Akasema, “Ni vema Isaya alivyonena juu yenu, akisema, ‘Mnayo macho na hamwezi kuona, masikio na hamwezi kusikia.’” Ni tamasha la kuchukiza, lakini hivyo ndivyo walivyokuwa.

²⁵ Na sasa tunaona karibu kitu kile kile kipo leo hii, wakati tunajua kwamba tunaishi katika saa ambayo giza kuu inabidi

lifunike dunia na watu. Pia tunakuta, kwamba mafanikio haya yote ya kisasa, ya wakati mkuu, na kadhalika, ambao tunaishi, ni ishara tu ya giza totoro katika hali ya kiroho. Tuko katika wakati wa kanisa la Laodikia, ambapo wao tu ni vuguvugu. Wangeweza kwenda kanisani, na watu hufanya hivyo, na—na kuonekana kuwa na bidii kwenda kanisani; ila kujua chochote kuhusu Roho, wakati wanaoishi, baadhi yao ni vipofu wawezavyo kuwa kuhusu mambo hayo. Haijalishi kile Mungu angefanya, na jinsi ambavyo kingethibitishwa vizuri na Neno Lake, bado hawawezi kabisa kukiona. Sijui kama si karibu tu vile alivyosema, “Tunayo macho, bali hatuwezi kuona.” Tunapaswa kuangalia kote na kuona mambo haya yote yanayotendeka ni ishara kwamba mwisho umekaribia, kwa sababu haya ndiyo mambo yaliyotabiriwa kuwapa kwenye wakati huo.

26 Ninawatakeni mtambue mwendeleo usiobadilika wa Neno la Mungu na kazi Zake. Mnaona, Yeye habadilishi mpango Wa—Wake. Yeye kamwe habadilishi njia Zake. Kikamilifu tu kabisa, Maandiko yako katika mwendeleo mkamilifu. Kila kitu afanyacho Mungu kiko katika mwendeleo na kile Yeye alichofanya. Unaona? Na kile alichofanya kwanza, hicho ni, Yeye atakifanya mara ya pili vivyo hivyo.

27 Na ili tu kuwathibitishieni, Yeye ameweka kanuni duniani. Na Yeye daima amewapa watu Wake ishara kabla ya tukio kutokea. Sasa Yeye amefanya hivyo daima. Na daima Yeye atafanya hivyo, kwa sababu Yeye ni Mungu asiyebadilika. “Mimi ni Mungu,” Yeye alisema, “Sina kigeugeu.” Jinsi Yeye anavyoweza mpango Wake mwanzo, hivyo ndivyo ulivyo katika kila wakati. Kamwe haubadilishi.

28 Alipouweka ulimwengu kugeuka kwenye msingi wa saa ishirini na nne; huenda tukawa na nyakati za kuokoa mwanga wa mchana, na kila namna ya nyakati, bali kamwe haubadilishi kugeuka kwa ulimwengu. Hufanya mzunguko wake mkamilifu kila saa ishirini na nne, hugeuka. Habadilishi majira, Mungu anayo majira ya kuchipua, wakati wa jua kali, wakati wa baridi kali, hakika tu jinsi ilivyokuwa. Hivyo ndivyo Yeye alivyofanya mara ya kwanza, hivyo ndivyo Yeye hufanya kila mara. Mwendeleo wa kanuni Zake, na wa Neno Lake, na wa kazi Zake, jinsi zote zinavyopatana tu kikamilifu!

29 Hivyo basi, kama tungeweza kuona kile kilichokuwa, tunaweza kujua kile kilichoko na kile kitakachokuwako. Unaweza kuwekea msingi mawazo yako juu ya hilo, kwa kuwa Andiko linasema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

30 Tunaona kabla ya majira ya kuchipua kuwadia. Tazama baadhi ya kanuni Zake. “Ukiona miti ikichipua,” Yeye alisema, “unajua kwamba majira ya jua kali yanakaribia.” Majira ya kuchipua ni dalili ya kuanza kwa majira yajayo ya jua kali. Hiyo ni kanuni. Daima hufanyika namna hiyo. Hamuwi na

jua kali, na halafu yapata wakati baridi kali inapoingia ndipo majani yanakuja. La, unakuwa na majani kwanza, kwa sababu ni utangulizi wa kanuni Zake za maumbile, kwamba majira ya kuchipua yanakuja. Kamwe haishindwi. Ukiona miti ikianza kuwa miororo, kote kwenye gome, na chipukizi ndogo zinaanza kuvimbisha, unajua kwamba ni ishara kwamba majira ya kuchipua yamewadia, yanaingia.

³¹ Ukiona majira ya kupukutika kabla hatujakuwa na jalidi wala chochote, nayo majani yanapukutika kutoka kwenye miti, unasema, “Vema, wakati wa mapukutiko umekaribia.” Unajuaje? Kwa sababu majani yanapukutika. Maumbile yanajiandaa kwa ajili yake. Kila mwaka ni vile vile.

³² Yeye pia hutupa ishara katika kubadilika kwa hali ya anga. Unaweza kutoka nje na utazame, kama Yeye alivyosema, “Ukiona mbingu ni nyekundu na kumetanda, kesho kutakuwa na dhoruba.” Na Yeye kamwe habadilishi hilo. Yeye daima hutuonya. Unaweza kuchukua, kuhisi hewa ikianza kuwa na unyevu, muda mrefu kabla ya dhoruba, na kuangalia maumbile yote yakiingiana moja kwa moja na hilo. Ni ishara.

³³ Kama ambavyo nimesema mara nyingi, “Kama hakukuwepo na Biblia, ningejua kulikuwa na Mungu, kuangalia tu jinsi maumbile yanavyofanya kazi.” Ni kanuni Zake, zote ziko katika mwendeleo moja na nyingine. Neno Lake liko katika mwendeleo; Hilo haliwezi kushindwa. Ishara Zake ziko katika mwendeleo na wakati. Ishara ziko sawasawa na Biblia. Ishara ziko moja kwa moja mwezini. Ishara ziko moja kwa moja angani. Ishara ziko moja kwa moja ardhini. Ishara ziko moja kwa moja kanisani. Na sisi tunaweza kuangalia kote kanisani, leo hii, na kuona ishara iko sawa kabisa Kwake kuja.

³⁴ Kwa mfano, jinsi inavyofanya kazi juu ya maumbile. Nimekuwa huko juu kwenye misitu ya kaskazini, mahali ambapo ninge kuwa ninawinda, kabla kamwe hatujawa na ki—kipindi cha baridi; maskini mabata wanatoka Louisiana, wanaenda huko juu na kutengeneza viota vyao, na kuangua vitoto vyao. Acha tu upepo wa kwanza baridi uje juu ya kilima hicho wakati theluji inafunika milima, na maskini mabata wainuke kutoka hapo, na kamwe hawajawahi kutoka kwenye hicho kidimbwi, na kuja moja kwa moja Louisiana wawezavyo kuja. Ni maumbile, unaona, kanuni za maumbile. Wanafanya hivyo kila mwaka. Na halafu hebu, muda si muda wajua, huku chini Louisiana jua kali linaanza kuangaza, chini hapa Louisiana, waangalie wote wakiwa pamoja, wanakutanika tena, na kuondoka moja kwa moja kuelekea milimani tena.

³⁵ Waangalie mabata bukini hapa Texas, ambapo wengi wao huenda. Nimeona wakati ambapo ingetubidi kusimamisha motokaa, kwenye barabara. Hawajisumbui kuhusu yeyote. Wanafikiria kuhusu kwenda. Wana uamsho unaoendelea. Wote

pamoja, hujawahi kusikia kelele kama hiyo. Ni mbaya kuliko Wapentekoste, wanapokusanyika pamoja. Unaona? Ni kitu gani? Ni kanuni za maumbile. Unaona, wao, kila mwaka wanakusanyika pamoja, kisha wanatembea katika kundi, kisha wanaondoka. Wakati hao mabata wakiondoka, na mabata bukini kuondoka Texas, majira ya jua kali yanakuja. Hiyo ni kweli.

³⁶ Ndipo wanapoondoka British Columbia ya kaskazini, majira ya baridi kali yanakuja; unawasikia hao mabata bukini wakienda, wakilia kwa nguvu kama wafanyavyo, wakienda kusini. Ninaweza kuwasikia na kulia, kwa sababu ninamwona Mungu akiwaongoza. Ni kitu gani kinachowaongoza kupitia hewani kusiko na njia, wakati yeye si kitu ila hayawani bubu? Ni kitu gani kinachofanya hivyo? Nikimsikia akiteremka, akilia, huyo kiongozi huko nje, kwa namna fulani akichukua njia yake; labda hajawahi kuruka kwenda Louisiana hapo kabla, bali atafika huko. Usifadhaikie. Anacho kitu fulani ndani yake kinachomwambia mahali pa kwenda. Yeye anaruka. Anaongoza kundi. Kundi lao lote linakuja. Huenda hawajawahi kuwa hapa hapo kabla. Lakini anajua hasa ambapo ma—mashamba ya mpunga yana mchele, sababu anacho kitu kinachomwongoza. Ni maumbile.

³⁷ Halafu majira ya kuchipua, wakati kukiwa shwari na joto chini hapa kupitia majira ya baridi, atarudi moja kwa moja tena. Kwa nini? Ni maumbile yakijionyesha yenyewe. Ni kanuni za Mungu.

³⁸ Ishara Zake daima hutangulia matukio Yake, kama tu hiyo ifanyavyo. Ukiona mabata bukini wakienda, uone chipukizi zikija, uone majani yakipukutika, unaona, ni mwendeleo wa maumbile yakiingia. Kanuni ya Mungu ya maumbile inaingia, na Yeye anatanguliza matukio Yake. Daima imekuwa, kamwe hajawahi kushindwa, na kamwe haitashindwa.

³⁹ Kama tukifuata tu mwendeleo wa Neno la Mungu, hatutashindwa kamwe, pia. Ikiwa hatutachukua m—mwelekeo wa kisasa wa siku hii na—na kujaribu kuingiza kitu kingine ndani yake, ila kufuata tu mwendeleo wake kwa ajili ya wakati huu, angalia kinachotukia. Tutaenda moja kwa moja nyumbani, pia, moja ya siku hizi. Daima hufanya hivyo, na kamwe haishindwi.

⁴⁰ Manabii ndio ishara kuu. Ishara kuu ya Mungu ni nabii. Sasa ninaenda kuzungumza dakika chache juu ya hilo. Hao ni Neno Lake lililodhihirishwa la wakati huo, na hiyo ndiyo sababu nabii daima ni ishara kuu ya Mungu. Yeye hajawahi kutuma hukumu juu ya nchi pasipo kwanza kumtuma nabii. Angalia tu, na uchunguze Maandiko. Nabii ndiye ishara kuu ya Mungu, kwa watu Wake, kwamba Yeye amemtuma mtu huyu, mtu huyu fulani, kama vile Nuhu, kama Musa, na—na Eliya na manabii.

Yeye huwatuma ili kudhihirisha Neno kwa ajili ya wakati huo, kuwapa watu Wake onyo.

⁴¹ Sawa tu na anavyotuma kipindi cha baridi juu ya mabata, kuwakimbiza kutoka Kaskazini kwenda Kusini; mwendeleo katika maumbile, mwendeleo katika Neno, Yeye kamwe hashindwi kufanya hivyo. Kama inahitaji hali ya baridi kuwapeleka chini, mwaka ujao inahitaji hali ya baridi kuwapeleka chini. Kama ikihitaji hali ya joto kuwarudisha, mwaka unaofuata inahitaji hali ya joto kuwarudisha.

⁴² Basi wakati Mungu anapokuwa tayari kutuma hukumu, kabla hajatuma hukumu, Yeye humtuma nabii na kudhihirisha Neno Lake, anathibitisha Neno la wakati huo. Alifanya hivyo katika vizazi vingine vyote. Aliahidi kufanya hivyo katika wakati huu. Na Yeye atafanya hivyo katika wakati huo, haijalishi kile watu wanasema juu yake. Yeye atafanya hivyo, kwa vyovyote vile, kwa sababu Yeye hawezi kuvunja mwendeleo Wake. Ndivyo Yeye alivyopanga, Yeye hulifanya vile vile. Yeye kamwe hashindwi kulifanya kama alivyolifanya kwa mara ya kwanza.

⁴³ Kama vile Yohana Mbatizaji, sasa, tulikuwa tumekuwa na miaka mia nne, kuanzia Malaki hadi Yohana, hakukuwa na ishara, nabii wa Agano la Kale, yapata kipindi kirefu (ila wakati wa waamuzi) ambapo kuliwahi kuwa bila nabii. Shida ilikuwa nini, ni kwa nini hawakuwa na nabii kwenye wakati huo? Hakukuwa na Neno lililowekwa kwa ajili ya wakati huo. Iliwabidi kungojea mpaka wakati unaofaa ukawadia. Iliwabidi kungojea. Unabii katika Malaki ulisema, ilikuwa Malaki 3, “Tazama, ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, ataiandaa njia Yangu mbele Yangu,” Malaki 3:1. Sasa, huo ulikuwa ni unabii wa Malaki wa kuja kwa Bwana Yesu. Hakuna kitu kilichopaswa kutukia kati ya wakati huo, kwa hiyo kanisa likawa tu wavivu na kuendelea kwa njia yake lenyewe, mpaka wakati wa ahadi ukakaribia.

⁴⁴ Ndipo wakati wa ahadi ulipokaribia, Mungu, katika njia ya kimbinguni, alimleta Yohana duniani. Alikuwa ni mtu aliyezaliwa na mwanamke, bila shaka, na sisi tunajua mama yake aliitwa “Elisabeti” na baba yake aliitwa “Zakaria.” Walikuwa watu wema. Na baba yake alikuwa ni kuhani. Ilikuwa ni kawaida kwa wavulana wa siku hiyo kufuata ka—kazi ya baba yao, lakini tunafundishwa kwamba Yohana, alipokuwa na umri wa miaka tisa, baada ya kifo cha baba yake, alienda nyikani na kukaa peke yake mpaka alipokuwa na miaka thelathini.

⁴⁵ Unaona, kama angalikuwa amegeukia kile baba yake alichokuwa nacho, wangelimvuruga kabisa hata asingalijua jinsi ya kumwona huyo Masihi wakati akija. Asingalimjua Yeye kamwe. Bali alikaa nyikani. Kama angalienda kwenye seminari, na mwelekeo wa wazo la baba yake, basi kila mmoja

wao angalisema, “Sasa, Yohana, tunafahamu kwamba wewe ndiwe unayeenda kumjua Masihi ajapo. Sasa, hivi hufikirii kwamba Ndugu *Nanii* hapa anatoshea tu maelezo ya mtu huyo kikamilifu? Vipi kuhusu Kayafa, kuhani wetu mkuu leo hii, hivi hufikirii yeye tu ni mtu wa ajabu?” Yote hayo ndani ya nia yake takatifu, asingaliweza kuliwazia sawasawa.

⁴⁶ Alienda nje nyikani, na kungojea! Kazi yake ilikuwa kubwa sana kushinda elimu. Kazi yake ilikuwa kubwa sana kushinda theolojia. Ilimbidi kumtangaza Masihi. Basi yeye alikaa nyikani.

⁴⁷ Angalia kuhubiri kwake. Kuhubiri kwake hakukuwa ni maadili ya—ya theolojia ya siku hiyo. Unatambua kwamba hakukuwa. Alizungumzia nini? Shoka kwenye mti, nyoka. Unaona, hayo ndiyo yote aliyojua. Alikuzwa nyikani. Hayo ndiyo aliyojua: nyoka, na miti, na mashoka, na kadhalika. Na hayo ndiyo yaliyowekewa msingi ujumbe wake, maumbile. Wakati aliposema, “Nyinyi kundi la nyoka, ni nani aliyewaonya kuitoroka ghadhabu inayokuja? Msiwazie kwamba mnyae Ibrahimu baba yenu, kwa kuwa Mungu anaweza kutokana na mawe haya kumwinulia watoto Ibrahimu. Na pia shoka limewekwa kwenye shina la mti; na kila mti usiozaa matunda mema unakatwa, na kutupwa motoni.” Kasema, “Kwa kweli mimi ninawabatiza na maji kwa toba. Lakini kunakuja Mmoja nyuma yangu ambaye sistahili kuvibeba viatu Vyake, Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu, na moto. Pepeto Lake liko mkononi Mwake; Yeye atasafisha kabisa uwanda Wake, na kuteketeza makapi kwa moto usiozimika, na kupeleka ngano ghalani.” Amina.

⁴⁸ Yupo mtu, nabii kwelikweli. Yeye alikuwa na ishara ambayo alikuwa hana budi kuitazama. Ndipo wakati alipomwona Masihi, alikuwa na hakika sana kwamba Yeye alikuwa anakuja katika siku yake, alikuwa na hakika sana. Loo, laiti Kanisa lingaliweza tu kupata mahali Pake pa hakika, laiti Hilo lingalijua tu mahali Pake katika saa hii! Kwa sababu, kulingana na Andiko, yeye alipaswa awe ndiye atakayemtambulisha Masihi, na alijua kwamba ilibidi Yeye awe duniani katika siku za unabii wake. Hivyo basi Yeye alikuwa anakaa karibu na mahali alipokuwa anahubiria, sana hata akasema, “Yupo Mtu aliyesimama miongoni mwenu sasa, ambaye hamumjui, Mtu miongoni mwenu sasa.” Alijua hilo. Yeye alikuwapo. Wakati ulikuwa umekaribia. Alijua hilo.

⁴⁹ Siku moja alitazama, akishuka chini kutoka Mbinguni... Ndipo akaona Nu—Nuru, kama hua akishuka kutoka Mbinguni. Na Yule Hiyo iliangaza juu yake, akasema, “Ninashuhudia kwamba huyu ndiye Mwana wa Mungu.” Aliona Hiyo. Kwani Yeye, nyikani, aliniambia, ‘Ambaye utamwona Roho akishuka juu yake na kukaa, huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.’”

⁵⁰ Alikuwa ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, aliyefunzwa na Mungu, na akamfanyia Mungu kazi, mpaka Mungu na yeye wakawa. . . Yeye alikuwa ni nabii, nalo Neno likamjia, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, ndani ya maji. Yeye alikuwa ndiye Neno kwa ajili ya. . . la Mungu, kwa ajili ya wakati wa unabii wa Malaki. Malaki alisema kungekuwa na mtu kama huyo, naye Yohana akaja jukwaani, nabii, kutimiza Neno la Bwana, kwa ajili ya siku hiyo. Kwa hiyo, hilo, yeye alikuwa ndiye ishara kwa Israeli, kama tu wangelijua ishara.

⁵¹ Hata wanafunzi walisema, “Ni kwa nini waandishi wanasema kwamba nabii lazima, Eliya hana budi kuja kwanza?”

Akasema, “Amekuja tayari, nanyi hamkumjua.”

⁵² Mungu huifanya kwa njia rahisi mno, ili tu kuichukua ile mbegu teule, mpaka wengine hawaioni kamwe. Hiyo ndiyo kweli.

⁵³ Ni mamajusi wangapi waliokuwa Babeli, wakisoma unajimu, wakati hawa mamajusi watatu walipojua kwamba wakati, ingawa, katika mfumo huo wa jua, wakati nyota hizo tatu zilipopangana, ilikuwa ni ishara kwamba Masihi alikuwa duniani? Walijua hilo. Waliliamini. Na wao ndio walioziona hizo nyota. Wengine wote hawakuziona. Zilikuwa katika mkusanyiko wao uliofaa, bali waliziona katika njia ambayo Mungu alikuwa ameziwasilisha kwao.

⁵⁴ Hivyo ndivyo Injili ilivyo leo hii. Inaweza tu kuonekana katika njia ambayo Mungu anaiwasilisha kwako. Na ikiwasilishwa kwako nje ya mwendeleo wa Biblia, basi si Mungu anayekuambia hilo. Amina. Huwezi kufanya Biblia kusema uongo. Ni Neno la Mungu lisilokosea. Nalo halina budi kukubaliana na mwendeleo Wake, Neno Lake lingine lote. Haliwezi tu kusema *hii* mahali pamoja, na *hii* kitu kingine; na kufanya *hii* hapa, gonga, tawanya. Yeye hugonga ndipo kila wakati, Neno hufanya hivyo, kwa hiyo inakubidi kulifanya katika mwendeleo wa Neno lingine lote. Hivyo basi, njia Yake daima imekuwa, katika Neno, kumtuma nabii kabla ya wakati huo, kabla Yeye hajafanya Neno Lake lithibitishwe.

⁵⁵ Sasa huenda tukazungumza hapa, kwa dakika moja, *nabii* ni nini. Sasa katika matamshi ya Kiingereza, kulingana na matamshi yake ya Kiingereza, inamaanisha “mhubiri.” Vema, hayo ni matamshi ya Kiingereza. Lakini katika matamshi ya Kiebrania, inaitwa “mwonaji.”

⁵⁶ Na mwonaji ndiye aliyekuwa na tafsiri ya Neno lililoandikwa, tena aliona kimbele mambo yaliyokuwa yanakuja. Ndipo alipozungumza kuhusu mambo yaliyokuwa yanakuja, na kuthibitisha kwamba alikuwa mwonaji, basi alijua. Walijua alikuwa na tafsiri ya kweli ya Maandiko, kwa sababu Mungu, kupitia yeye, alidhihirisha Andiko lililoandikwa kwa ajili ya

siku hiyo. Amina. Usiwe mzembe. Amka! Huo ulikuwa ndio utambulisho dhahiri, mwonaji, mtabiri na msema kimbele. Na njia ya pekee ambayo walijua alikuwa anapata tafsiri ya kweli kwa Maandiko, kwa sababu yale aliyosema yalikuja kutimia. Ndipo walijua alikuwa ameitwa na Mungu, Mungu alisema hilo. Ndipo basi wakatambua kwamba yalitimia, yalikuja moja kwa moja katika mwendeleo na Neno kwa ajili ya siku hiyo.

⁵⁷ Yesu alisema, “Yachunguzeni Maandiko!” Wakati walipoona kwamba Yeye aliweza kutambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwao, na wakamwita Beelzebuli, Yeye alisema, “Yachunguzeni Maandiko, Hayo ndiyo Ambayo yananishuhudia Mimi.” Mwendeleo wa Maandiko yakienenda kikamilifu na ishara ya wakati! Yeye alikuwa ni ishara ya Mungu ya wakati. Alikuwa ndiye dhihirisho la Neno lililoandikwa, na pia angeweza kutabiri kile ambacho kingetendeka, nao wasingeweza kukikana. Alikuwa ndiye ishara kuu ya siku hiyo. Hakika alikuwa.

⁵⁸ Angalia mwendeleo wa Neno Lake lisilobadilika, pia Roho Mtakatifu. Yesu alisema, “Wakati Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu, Yeye atawakumbusheni, au kufunua mambo haya ambayo nimewaambia, na pia atawaonyesha mambo yanayokuja.” Sasa Biblia . . .

⁵⁹ Watu wanasema leo hii, “Hakuna kitu kama nabii, ulimwenguni.”

⁶⁰ Vema, ni kwa nini Paulo akaiweka kanisani? “Kulikuwa kwanza mitume, manabii, walimu, wachungaji, na wainjilisti.” Hakika, kulikuwako.

⁶¹ Roho Mtakatifu ndiye Nabii. “Wakati Yeye Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu, Yeye atafunua, au kuwafundisha, kuwaonyesha. Mambo haya niliyowaambia yamekuwa yote ni kitendawili, hamyaelewi sasa kwa sababu si kwa ajili ya wakati wenu sasa. Lakini atakapokuja Roho Mtakatifu, Yeye atayafanya mambo hayo yaishi, moja kwa moja kwa ahadi. Si hayo tu, bali atawaonyesha mambo yajayo.”

⁶² Utukufu! Mwendeleo wa Neno la Mungu, ahadi ya Mungu, Roho wa Mungu. Tunaishi kwenye saa, tukiona kufunuliwa kwa utabiri wa wakati huu, ukitimia. Ni wakati mkuu jinsi gani tunaoishi! Roho Mtakatifu alikuwa atuonyeshe mambo yaliyokuwa yanakuja.

⁶³ Mwanadamu daima amejaribu kufanikisha na kujitengenezea jina kwa kujiundia mwenyewe ishara kuu. Ni kitu gani kinachomfanya mwanadamu kujaribu kujitengenezea mwenyewe kitu kikuu kuliko yule mwingine? Ni kwa nini yeye hufanya hivyo? Kwa sababu, ndani yake, yeye ni maumbile. Yeye, kwa asili, yeye ni mwenye dhambi, lakini katika maumbile yeye ni Mwana wa Mungu aliyanguka.

⁶⁴ Ni kwa nini yeye hujijengea nyumba ya kupendeza namna hiyo, akiiboresha kila wakati? Ni kwa . . . Ndege

hatengenezi makao yake tofauti hata kidogo. Nguruwe wa nchini angali anaishi ndani ya ardhi, kama alivyofanya miaka elfu moja iliyopita. Unaona? Ndege angali anajenga kiota kama alivyofanya miaka elfu moja iliyopita. Unaona? Lakini mwanadamu anaendelea. Kwa nini? Yeye ni...na yeye—na yeye ni mwana wa Mungu aliyeanguka. Kuna kitu ndani yake kinachomwambia kwamba ikulu, inayopendeza zaidi, na kuna kitu ndani yake kinachojaribu kukipata. Kinatafuta kitu hicho. Loo, tukiangalia baadhi ya nyumba hizi leo, zitakuwaje upande ule mwingine? Wakati maumbile yaliyoanguka yanaweza kufanya jambo kama hili, itakuwaje?

⁶⁵ Lakini hilo ndilo linalomfanya kufanya hivyo, asili yake ndani yake. Ingawa ameanguka, anajaribu kufanya jambo fulani mwenyewe. Anajaribu kufanya hilo. Imekuwa tangu mwanzo.

⁶⁶ Adamu, alijaribu kuunda dini kuu bila ya upatanisho. Wangali wanajaribu kufanya hivyo. Dini kuu, kuunda dini ili aweze kuishi vyovyote alivyotaka, pasipo na upatanisho, na angali awe na kifuniko. Alijaribu kulifanya hapo mwanzo, na angali anajaribu kulifanya.

⁶⁷ Lakini njia ya Mungu iliyotolewa ilikuwa ni upatanisho, na kamwe haitafanya kazi vinginevyo. Haina budi kurudi kwenye upatanisho.

⁶⁸ Nimrodi alijaribu kujenga mnara mkuu, mnara wa kidini. Kama kutakuwa na mtu yeyote ambaye angeninii... Mnara mdogo ungekuwa labda na urefu wa futi thelathini, bali alitaka kufanya jambo kuu, kitu kikubwa zaidi, kwa hiyo alijijengea mnara. Hiyo ilikuwa katika siku yake.

⁶⁹ Nebkadreza alitaka kujenga jiji kuu. Alichukua mfano kutoka Mbinguni, mabustani yanayoning'inia, mto Frati, karibu na kiti cha enzi; kama vile tu Maji ya Uzima, Mto wa Uzima, unaoteremka karibu na Kiti cha Enzi cha Mungu. Alijaribu kujenga jiji kuu.

⁷⁰ Marekani, miaka michache iliyopita, ilijaribu kutengeneza meli kuu. Waliitengeneza, kwa hiyo wakasema, “Kamwe haitazama. Isingeweza kuzamishwa.” Mungu aliweka Titanic chini ya bahari. Inaonyesha kwamba mafanikio ya mwanadamu hayatafaidi chochote. Yote ni vumbi na inarudi kwa vumbi, kilicho ndani yake.

⁷¹ Urusi, leo hii, inajaribu kumwinua mwanasayansi mkuu anayeweza kufanya mambo fulani ya kisayansi, kuuteka ulimwengu.

⁷² Ufaransa, si muda mrefu uliopita, ilidhanja wangali wangeweza kuwa na wanawake wao, wanywe mvinyo, na wakati mzuri; kwa hiyo wakajitengenezea wenyewe, Ngome ya Maginot, ilivyoitwa, wakawa na bunduki zao zote zimeelekezwa Ujerumani, adui mkuu. “Kama wakiwahi kuja upande huu! Tutaishi tu vyovyote tutakavyo. Nasi tutajenga ngome kubwa

hapa nje, tuitengeneze kwa saruji, tuelekeze bunduki zetu. Kama wakiwahi kuja, tutagusa kitufe; itafyatuka na kuwalipua kurudi huko Ujerumani.” Ujerumani ikatembea taratibu nyuma ya hiyo. Walisahau.

⁷³ Vivyo hivyo nasi tumesahau! Mungu, kwa mkono Wake wenye nguvu, anaonyesha ulimwengu huu hauwezi kusimama. Bali wanataka ishara kuu.

⁷⁴ Walijitengenezea Ngome ya Maginot, na Ujerumani ikatembea taratibu nyuma yake, kwa sababu walisahau. Kwa hiyo, waliweza kuweka bunduki kwenye bonde la chuma lenye mizinga, wangeweza kuigeuza upande ule mwingine na kupiga risasi. Walisahau hiyo.

⁷⁵ Hilo ndilo kanisa linalosahau leo hii. Wanalo kanisa kuu. Wanalo dhehebu kuu. Wanao watu waliovalia kwa njia kuu. Wanacho kila kitu watakacho, na wahudumu wakuu wenye elimu kuu. Bali mnasahau kwamba Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Halina budi kuja jinsi Mungu alivyosema lilikuwa linaenda kuja. Hakuna njia ya kulihepa.

⁷⁶ Moja kwa moja ukaja Ujerumani, baadaye. Walifikiria hilo lilikuwa ni wazo jema, kwa hiyo wangeweza kuitengeneza ili waweze kugeuza bunduki zao upande ule mwingine. Kwa hiyo walijijengea ngome, iliyoitwa Ngome ya Siegfried, lakini makombora ya Marekani ya kuangamiza kila kitu yaliwalipua kutoka ardhini. Unaona?

Wanajaribu kutengeneza kitu kikuu, kikuu, kila wakati.

⁷⁷ Mekanisa leo hii wanataka dhehebu lao kuu. Tumejaribu kwa muda mrefu, Wamethodisti wanachukua yote, Wabaptisti wanachukua yote. Ndipo Wapentekoste wakaja katika mashindano, wanachukua yote. Wakatoliki wanajaribu kuchukua yote. Kwa hiyo wanakuta, kundi dogo lililotawanyika, hawawezi kufanya hivyo. Lakini waweke pamoja, jinsi linavyosikika la Kimaandiko! “Tuweke pamoja! Tuweke pamoja, tutalifanya basi. Tutatorosha ukomunisti hadi baharini.”

⁷⁸ Bila kujua kwamba Mungu aliinua ukomunisti kuwashinda. Hilo ni neno kubwa kwa mhubiri kusema. Lakini ninachefuka sana kusikia hili, “Ukomunisti! Ukomunisti!” Mnajua ishara za ukomunisti. Bali saa mnayoishi, hamjui chochote kuihusu. Hivi hamjui kwamba Mungu aliahidi kufanya hilo? Sawa na Yeye alivyoanza, kumwinua Nebkadreza kuangamiza Israeli, kwa sababu hawakutembea katika njia Yake. Biblia inafundisha hilo dhahiri, na hii ndiyo saa kwa ajili ya hilo kutendeka.

⁷⁹ Tunapata, katika siku tunayoishi, mambo haya yote. Wao si kitu chochote kilichofichika, ni kitu ambacho Mungu amefunua katika Neno, ila watu ni vipofu sana hawawezi kuliona.

80 Leo hii tunawazia, “Vema, sasa, ikiwa sote tunaweza kuunganika katika umoja uliopo, au katika baraza, ‘wingi wa mashauri kuna usalama.’”

81 Hiyo ni kweli, lakini ni umati wa aina gani unaoshauriwa nao? Mnawezaje kutembea pamoja? Unawezaje kuleta madhehebu haya pamoja? Baadhi yao waaminio, na wengine wasioamini, na wengine wanaojifanya waaminio, unaendaje kuwaweka pamoja na kutembea pamoja? “Wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana?” pia imeandikwa. Angalia hapa wafanyalo, wanajiundia umati.

82 Wakati mmoja walifanya jambo lilo hilo katika Biblia, wakati Ahabu alikuwa taabani, na, ama Ahabu aliagizia Yehoshafati aje kutoka—kutoka Uyahudi na—na kutafuta kujua kama angeweza kuchukua majeshi yake na kumsaidia kupiga vita. Naye Yehoshafati, mwaminio nje ya muunganiko na Mungu wake, aliteremka huko chini na kusema, “Naam.”

83 Kasema, “Kuna sehemu ya nchi huko ambayo ni yetu. Hiyo ni yetu. Mungu alitupatia hiyo. Nabii Yoshua alitugawia nchi hiyo, na sasa tunaona kwamba ni mali ya adui. Adui anakuza ngano hapo, inayopaswa kuingia katika matumbo yetu Waebrania, na sasa wanainyakua huko na adui.” Kasema, “Hivi tutakwea? Utakwea pamoja nami?”

84 Vema, sasa, Yehoshafati, bila kuchukua wazo la pili, kasema, “Mbona, hakika. Magari yangu ni magari yako. Wapanda farasi wangu ni wapanda farasi wako. Watu wangu waendao kwa miguu ni watu wako waendao kwa miguu. Sisi ni ndugu. Hebu tupatane, tutafanya mwungano na tutakwea.” Ndipo ikamwingia moyoni, “Heri tumtafute Mungu, kwanza.” Loo, jamani!

85 Kabla ya kujiunga na kitu hicho, afadhali umtafute Mungu, kwanza. Afadhali uchunguze kabla ya kutupa kanisa lako katika Babeli kama hiyo. Itakubidi kufanya hivyo, ama au uchukue alama ya mnyama. Lakini endelea.

86 Wakasema, Ahabu akasema, “Hakika, nilipaswa kuwa nimewazia hilo.” Kasema, “Ninao mia nne hapa chini kwenye seminari, manabii wa Kiebrania, bora kuliko wote walioko nchini. Hakuna aliye bora, popote. Tutaenda tuwalete.”

87 Ndipo wakaja manabii, na wote wakatabiri. Hakika, walikuwa hasa na—na wazo jema, walidhania. Wakasema, “Hakika, hiyo ni mali ya Israeli. Kama Mungu aliwapa hiyo Israeli, ni mali ya Israeli.”

88 Lakini Mungu hukupa tu vitu hivi kwa masharti. Hilo ndilo ninalowazia kuhusu vipawa vya Roho, Kanisani, leo hii. Wengi sana husema kinapaswa kuwa mle ndani. Lakini kitakuja tu humo ndani chini ya masharti.

⁸⁹ Mhudumu maarufu aliniambia, si muda mrefu uliopita, “Hivi hutaacha kuwakemea wanawake na wanaume, kuhusu *hiki, kile, au kinginecho?*” Kasema, “Wangekuchukulia kama mwonaji, au nabii.” Kasema, “Kwa nini usiwafundishe jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu na vipawa vikubwa?”

Nikasema, “Watafanya nini navyo?”

⁹⁰ Kasema, “Wewe, unapaswa kuwafundisha mambo bora kuliko kujaribu kuwaambia jinsi ya kukata nywele zao na kuvalia nguo zao, na kadhalika namna hiyo. Hupaswi kufanya hivyo.”

⁹¹ Nikasema, “Ninaendaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatasikiliza ABC zao?” Unaona? Unaendaje kufanya hilo? Wana ninii . . . Mungu hutoa vipawa hivi kwa masharti.

⁹² Na nchi hiyo ilikuwa ni mali ya Israeli, katika masharti kwamba walidumu waaminifu kwa Mungu. Lakini angalia haini waliyekuwa naye pale kwa ajili ya mchungaji, akiruhusu tu uabudu sanamu na kila kitu kingine kufagiliwa ndani. Bali manabii, wakifikiria kwamba hiyo ilikuwa ni ya Mungu, ilikuwa ni ya Israeli, ilikuwa ni zawadi kwa Israeli, walipaswa kuimiliki.

Hilo ndilo jambo lile lile linalotendeka leo hii.

⁹³ Lakini kumbuka wakati wote walipotabiri kwa nia moja, na mmoja wao, ninaamini, Zedekia, alijitengenezea jozi kubwa ya pembe za chuma. Akasema, “Utachukua hizi na kuwasukuma Washami moja kwa moja kutoka nchini, kwa hizi.”

⁹⁴ Na hilo halikumfaa kabisa mtu huyu mwema, mwadilifu, aliye wa kidini, Yehoshafati. Akasema, “Vema, hivi huna mwingine mmoja?”

⁹⁵ “Mwingine mmoja, wakati tuko na mia nne? Mia nne, wakiwa na nia moja, wanasema, ‘Tutakuwa na Baraza la Makanisa. Tuta—tutafanya tu hivyo.’” Unaona, wote walikuwa katika umoja. Kasema, “Wako, kila mmoja, katika makubaliano.” Kasema, “Kwa nini usiendeleo basi na kukwea tu pamoja nami?”

⁹⁶ Akasema, “Hivi hakuna mwingine mmoja tu ambaye ungeweza kumtaka ushauri kuhusu hili, aliye na muungano na Mungu?”

⁹⁷ Akasema, “Naam, yuko mwingine mmoja, bali kwa kweli ninamchukia.” Jambo ndilo hilo.

⁹⁸ “Loo, hebu mfalme asiseme hivyo,” kasema Yehoshafati. “Hebu—hebu twende tukamtake ushauri na—na tuone itakuwa ni kitu gani.”

⁹⁹ Akasema, “Yuko mmoja, naam, ninamjua, mwana wa Imla,” kasema, “Mikaya. Ila,” kasema, “Ninamchukia.” Kasema, “Yeye daima huniwekea laana juu yangu. Yeye daima huniambia kuwa niko makosani na—na kuzimu kunaningojea.” Kasema,

“Ninachukia hata kumsikia akihubiri. Hakuna mmoja wa hao wahudumu wengine hata hawatamkaribisha makanisani mwao.” Kasema, “Tumemtupa nje, muda mrefu uliopita, kutoka katika muungano.” Kasema, “Hata sijui mahali ungeweza kumpata.”

“Loo,” akasema, “mfalme na asiseme hivyo. Hebu twende tukamwite.”

¹⁰⁰ Kwa hiyo mmoja kutoka kwa muungano akaenda kumtafuta. Akasema, “Sasa, Mikaya, una nafasi ya kurudishiwa kadi yako ya uwanachama tena, kama utasema jambo lile lile wanalosema. Unaona, ikiwa tu utafanya hivyo, kama utakubaliana na sisi, kwamba sote tunapaswa kujiunga na baraza na sote tuingie pamoja, tutaninii tu. . . utakuwa mmoja wetu.”

¹⁰¹ Loo, lakini Mungu daima anaye mtu atakayesimama mkweli. Alisema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu kile Yeye anachoniambia niseme.” Amina.

¹⁰² Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Yehoshafati. Mnajua jinsi hadithi hiyo inavyoenda. Ndipo akasema, “Mbona, Mungu alisema!” Ingawa mia nne katika baraza walikuwa kinyume chake, hata hivyo alisimama. Nayo ilikuwa ni ishara kwa Yehoshafati. Na Yehoshafati asingalienda huko nje.

¹⁰³ Kwa hiyo tunaona jinsi matokeo yalivyokuwa, kwa sababu kwamba neno la mtu huyo lilikuwa hasa na neno la nabii lililokuwa limetabiriwa kwa ajili ya siku ya Ahabu, “Kwa sababu alimchukua Nabothi mwenye haki na kumwua, na kadhalika, Mungu alimwambia, kupitia nabii Eliya, kwamba, ‘Mbwa watairamba damu yako mwenyewe,’ hiyo ni kweli, na kile ambacho kingetukia, na jinsi ambavyo wangemla Yezebeli.” Alitabiri. Hilo lilikuwa ndilo Neno, naye Mikaya alikuwa ndiye ambaye angelifanya kutimia. Amina.

¹⁰⁴ Yeye alikuwa ni nabii ishara kwa ajili ya siku hiyo, laiti tu wanalimsikiliza yeye. Kamwe haijawahi kushindwa. Mungu daima huituma.

¹⁰⁵ Kila mtu daima anataka ishara. Tunapaswa kutafuta ishara. Hiyo ni kweli. Bali ya kidini. . . Ishara za Kimaandiko, si ishara za kidini; ishara za Biblia.

¹⁰⁶ Kila mtu alikuwa anaenda kutafuta ishara, nao walijua hii ingekuwa ni siku kuu, Mungu akiona mwisho tangu mwanzo, kwa hiyo Yeye akasema, “Nitawapa ishara, ishara kuu. Nitawapa ishara ya Milele.” Amina. “Nitawapa moja ambayo haitashindwa kamwe na haitapita kamwe.” Amina. “Wanataka ishara, kwa hiyo nitawapa moja, ishara kuu.”

¹⁰⁷ Hakuja katika umaridadi wa ulimwengu, jinsi walivyomtarajia Yeye kuja. Lakini Yeye alisema nini? “Bikira atachukua mimba.” Amina. Hiyo ilikuwa ni ishara. Hiyo ilikuwa ni ishara kuu. “Bikira atachukua mimba.” Amina.

Ninii kuu, ishara kuu; si ishara ya kawaida, bali ishara kuu; bikira akichukua mimba, unaona, ishara ya kimbinguni. Ya kimbinguni! Ilikuwa ni ishara kuu, kwa kuwa bikira hakuwahi kufanya hivyo hapo kabla, lakini, "Atachukua mimba."

¹⁰⁸ Ilikuwa iwe ni kitu gani? "Jina Lake litaitwa Imanueli." Itakuwaje? "Mungu na mwanadamu watakuwa mmoja." Hiyo ndiyo ishara kuu.

¹⁰⁹ Ee Mungu, laiti ulimwengu ungeweza tu kuona hilo, kwamba Mungu na mwanadamu ni mmoja! Ishara kuu ilikuwa ni yule Mtu wa kwanza ambaye Mungu angeingia ndani yake; yote aliyokuwa Mungu Yeye alimimina ndani ya Kristo. Na yote aliyokuwa Kristo alimimina ndani ya Kanisa. Ishara kuu, Mungu na mwanadamu, pamoja, hiyo ilikuwa iwe ndiyo ishara kuu ya siku ya mwisho, wakati Biblia yote ilipaswa kutimizwa katika siku za mwisho.

¹¹⁰ Ishara kuu, "Bikira atachukua mimba. Na mimba hii, wakati Hiyo itakapozaliwa, itakuwa ni Mungu akidhihirishwa katika mwili," ishara kuu. Wangali hawaiamini, lakini ilikuwa hata hivyo. Ingali ni ishara kuu.

¹¹¹ Tazama, ishara kuu! Wanaye mtu mkuu leo hii, wanazo hadithi za kubuni za mtu mkuu, aina hizi zingine zote za vitu vikuu. Lakini Kanisa linayo ishara kuu, Mungu akirudi Kanisani tena, amedhihirishwa katika mwili wa mwanadamu. Mungu akiunganishwa na mwanadamu, ishara Yake kuu ya hakika!

¹¹² Angalia ishara ya Milele, ishara isiyoshindwa, Hiyo haitashindwa kamwe. Mwanadamu na... Neno na mwanadamu walifanyika mmoja. Wakati Neno la Mungu na mwanadamu walifanyika mmoja, kama vile Yohana Mt. sura ya kwanza isemavyo, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa katikati yetu," hiyo ndiyo ishara kuu.

¹¹³ Loo, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara kuu ya siku hiyo, wakati Roho yule yule aliyekuwa juu ya Yesu Kristo akija katika Kanisa Lake, kudhihirisha Neno liloandikwa kwa ajili ya siku hii, hiyo ingali ni ishara kuu.

¹¹⁴ Kanisa linaweza kuwa na ishara ya Baraza, wote wakija pamoja kwa ajili ya amani bandia ya ulimwenguni, na yote wanayotaka kuwa. Wabaptisti wanaweza kusema, "Tumepata milioni moja zaidi katika mwaka wa '44." Wamethodisti wanaweza kufanya kila namna ya majigambo watakayo, Umoja, au Utatu, chochote kile walicho.

¹¹⁵ Lakini ishara kuu ingali, ni, Mungu anabaki mkweli kwa ishara hiyo kuu: ni Mungu ndani ya mwanadamu, akidhihirisha Neno Lake lililoandikwa. Neno Lake, "Wakati Yeye Roho Mtakatifu akija juu yenu, atayafunua mambo haya, awaonyesheni, na atawaonyesha mambo yajayo." Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Hakika.

¹¹⁶ Uzao mkuu wa Ibrahimu, Yeye alikuwa, Mwana mkuu. Ibrahimu alikuwa na mwana mmoja, alimzaa huyo kwa mwili wa kawaida, huyo alikuwa ni Isaka. Ndipo akawa na Mwana mwingine, na huyo Mwana alikuwa kwa imani, huyo alikuwa ni Yesu; Yeye alikuwa ni Mwana wa Ibrahimu, Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu. Aliiona kimbele katika ono. Imani katika Neno Lake lililoahidiwa, ilionyesha katika ninii ya mwisho. . . kuonyesha, katika siku hizi za mwisho, Ibrahimu. Tunapaswa kuwa Uzao wa Ibrahimu. Kama tumekufa ndani ya Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu; na warithi pamoja na Yeye, kulingana na ahadi. Sasa, ni kwa nini Ibrahimu alipewa ishara hii kuu? Kwa sababu kwamba ingelea ishara kuu ya siku ya mwisho. Haina budi kuonyeshwa.

¹¹⁷ Mungu alimwonyesha Ibrahimu mwisho tangu mwanzo, na kile kilichokuwa kinaenda kutukia; Mungu akidhihirishwa katika Mtu, Mwana Wake mkuu wa imani. Mtu ambaye asingeweza kumwangamiza huyu Mwana; wangeweza kumwangamiza Isaka, wangeweza kumwangamiza Yakobo, na warithi baada yao, lakini huyu Mwana mkuu asingeweza kuangamizwa. Ibrahimu, Uzao wa Ibrahimu, imani hii, kwamba, si uzao wa kimwili, bali imani ambayo Ibrahimu alipokea, si kwa torati ya tohara; bali kwa imani katika Neno, Mwana mkuu wa imani ya Ibrahimu, ambaye alikuwa ni Yesu Kristo. Sasa, wana wake wengine wote walikufa, bali Mwana huyu asingaliweza kuuawa. Yeye aliuawa, bali asingekaa mfu. Kaburi halikuweza kumweka. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹¹⁸ Angalia Mwanzo 22:16 na 17, juu kwenye mlima ambapo Mungu alimwonyesha Ibrahimu kwenda, na huko aliona kondoo dume aliyeshikwa kwa pembe zake, nyikani. Tazama, upesi sasa. Baada ya kumchukua Isaka na kumfunga, ambaye alikuwa ni mwana wake wa kimwili, akamlaza juu ya madhabahu, kuondoa uhai wake; na ndipo alipoanza kuondoa uhai wake, katika utii wa upendo kwa Mungu. Ndipo, wakati alipofanya hivyo, jambo fulani likatukia. Alisikia Sauti, ikisema, "Ibrahimu, ondoa mkono wako, kwa kuwa ninajua kwamba wewe wanipenda Mimi." Ndipo basi akamsikia ko—kondoo dume akilia, ameshikwa na pembe zake nyikani, nyuma yake. Ndipo akaita jina la mahali hapo Yehova-yire.

¹¹⁹ Tazama, Mungu alisema, "Na uzao wako," uzao wa Ibrahimu sasa, "utamiliki malango ya adui zake." Yeye angeyachukua malango, ayamiliki malango. Yeye aliahidi hilo. Sasa, uzao wake wa kimwili ulifanya hivyo hakika. Wote wa uzao wa Ibrahimu wa kimwili walikuwa ni manabii waliokuja nyuma yake.

¹²⁰ Kulikuwa na Musa, uzao wa Ibrahimu, na, alipokuwapo, alifika kwenye lango, katika wajibu wake. Alifika kwenye lango la Bahari ya Shamu, baada ya kuwafundisha watoto wa Israeli kuhusu nchi ya ahadi ambayo Mungu alikuwa ameahidi. Alikuwa ni nabii wa Mungu. Alikuwa amedhihirishwa mbele

za watu, kama nabii wa Mungu. Mungu aliumba, kupitia yeye. Mungu alifanya kila namna ya ishara na miujiza, kupitia yeye. Na yeye alidumu moja kwa moja na Neno la Mungu, kwa sababu alimtafuta Mungu, kwanza. Na yeye alijua mahali pake. Alijua kwamba alizaliwa kwa ajili ya wakati huo, kudhihirisha Neno la Mungu kwenye wakati huo. Ndipo basi, moja kwa moja kwenye wajibu, alikumbana na kitu ambacho hakujua la kufanya, hicho kilikuwa ni Bahari ya Shamu. Vema, kulifanyika nini? Uzao wa Ibrahimu uliahidiwa kumiliki malango ya adui. Kwa hiyo wakati Bahari ya Shamu ilipokuwa lango ambalo asingaliweza kupita, Mungu aliingia jukwaani na kuchukua lango na kuondoka nalo, ndipo Musa akatembea kuvuka bahari juu ya nchi kavu. Uzao wake ulimiliki lango.

¹²¹ Wana wa Kiebrania walimiliki malango ya tanuru ya moto ambayo haikuweza kuwateketeza.

¹²² Danieli alimiliki malango ya adui kwenye vinywa vya simba ambavyo havikuweza kufunuliwa ili kumla.

¹²³ Samsoni, siku moja alinaswa kwenye...Kundi la watu lilikuwa limemzingira ndani ya mji. Ndipo, wakati alipofanya hivyo, aliyavuta hayo malango makubwa kutoka kwenye miamba, akayaweka mabegani mwake na kutembea kwenda kwenye kilele cha kilima. Kwa nini alikuwa hivyo? Alikuwa angali katika agano, vishungi vyake vilikuwa vingali vinaning'inia juu yake. Ahadi ilikuwa ingalipo, "Na yeye atamiliki malango ya adui wake." Amina. Hakika, bila shaka.

Hawa wote walikufa, askari hodari wa imani. Wote walikufa.

¹²⁴ Ndipo akaja jukwaani Uzao mkuu wa Ibrahimu, Uzao wa kifalme, Uzao mkuu, wa kifalme, Yesu Kristo, ambaye alikuwa ni Mwana wa Ibrahimu wa imani; ambaye alimwona kwa imani, kupitia ahadi ya Mungu, kwamba yeye angewabariki wote, awe baba wa mataifa mengi. Uzao wake mkuu ulikuja jukwaani.

¹²⁵ Hawa wengine walifanya nini? Walimiliki malango ya simba, malango ya moto, malango ya bahari, malango ya mji. Na kila mahali walipokuja, waliweza kumiliki malango kwa sababu waliahidiwa hilo. Bali, ilipofikia mauti, wote iliwabidi kufa.

¹²⁶ Sasa huyu hapa anakuja Uzao wa kifalme. Sio tu kwamba Yeye alimiliki malango ya adui, lakini Yeye alimiliki malango ya kifo, kuzimu, na kaburi, akafufuka siku ya tatu na kuifungua njia; akapasua pazia kutoka juu hadi chini, na kufanya njia kwa kila mwanamume na mwanamke ambaye alitamani kuja Kwake, angeweza kuja. Yeye aliyamiliki malango. Sio tu kwamba Yeye alifanya hivyo; bali wale waliokuwa wamekufa, katika imani, Yeye aliwateka mateka, akapaa Juu, na akawapa wanadamu vipawa. Huyu ni Uzao mkuu wa Ibrahimu. Huyu ni Uzao wa kifalme, Yesu Kristo, ishara kuu. Kumbukeni, ilikuwa ni ishara ya milele, ishara ya milele ya kimbinguni, Yesu alikuwa.

Alifufuka kutoka kwa wafu, wasingaliweza kumshikilia. Kifo, kuzimu, wala kaburi, havingeweza kumshikilia.

¹²⁷ Waebrania 13:8, kama nilivyosema, “Ni yeye yule jana, leo, na milele,” kuonyesha, kuonyesha ishara hii kuu katika wakati huu.

¹²⁸ Tazama, hebu tuchukue njia ya Ibrahimu, kwa dakika moja tu, mfano wa uzao wake. Ibrahimu, nabii, tazama. Mungu alikuwa amenena na yeye kwa njia nyingi tangu alipoondoka Ukaldayo, mji wa Uri. Alikuwa amesafiri kote. Na Mungu alikuwa amemwonyesha ishara nyingi kuu, akamtokea, akamwonyesha namna zote za mambo ambayo yangetukia, akamwambia kile ambacho kingetukia. Mambo haya yote Yeye alikuwa amemwambia. Lakini kabla hajampokea mwana wake aliyeahidiwa, alikuwa amesimama karibu na malango ya Mataifa, juu kidogo ya Sodoma. Na kabla hajapokea mwa—mwana wake mkuu, ama mwana wake aliyekuwa azaliwe mwana mkuu, bila shaka, kabla hajampokea (si Yule wa kifalme sasa), lakini, kabla hajampokea, alipokea ishara kuu.

¹²⁹ Ilikuwa ni kitu gani? Mungu alimshukia, katika umbo la Mtu. Tazama Mtu yule aliyezungumza na yeye, ambaye alisimama kwenye hema mahali alipokuwa na kufanya ishara kuu.

¹³⁰ Basi wakati Mwana wake mkuu alipokuja jukwaani, Mwana wake mkuu aliifanya ishara iyo hiyo, kuonyesha kwamba Yeye alikuwa ni Uzao mkuu wa Ibrahimu. Utukufu!

¹³¹ Pia aliahidi jambo lilo hilo katika siku za mwisho. Mnaona ninalomaanisha? Ibrahimu, kabla, kabla tu ya mwana aliyeahidiwa kuwasili; kama tunavyotazamia sasa, Uzao wa Ibrahimu, Uzao wa kifalme. Huo ulikuwa ni uzao wa kimwili; huu ni Uzao wa kifalme. Wakati uzao wa kimwili ulipopata ishara yao, wao—wao waliikataa; ndivyo na, itaninii. . .hakuna kitu ila Uzao wa Kifalme, bado mbegu hiyo ya kanisa itaikataa Hiyo tena. Daima wamefanya hivyo. Bali, tazama, ilikuwa ni ishara ya namna gani?

¹³² Hebu tutazame tu na tuone kile ishara kuu ilichokuwa. Kulikuwa na Mtu aliyekuwa, watatu wao. Na hivi ulitambua, wakati—wakati Ibrahimu alipowaona watu watatu wakija, yeye aliondoka na akasema, “Bwana wangu, hivi Wewe utanipita? Karibu ndani na uketi. Hebu nichote maji kidogo na kukutawadha Wewe miguu. Na upate kipande cha mkate, halafu uendelea na shughuli Zako.” Aliwaona watatu wakija, na kuwaita hao watatu, Mmoja, “Bwana.”

¹³³ Lutu, kanisa la kawaida, chini—chini huko Sodoma, aliwaona wawili wakija, ndipo akasema, “Bwana zangu.”

¹³⁴ Ibrahimu alijua “hawa watatu ni mmoja.” Kulikuwa hakika na Mmoja tu, kwa hao. Tazama, wawili kati yao walienda huko chini Sodoma, na Mmoja akabaki na yeye. Yeye akasema,

“Bwana wangu.” Tazama Yule aliyekaa na yeye; Ibrahimu, akiwa ni mfano wa aliyelitwa atoke, asiye ndani ya Sodoma, mteule kwa ajili ya wakati huo.

¹³⁵ Sasa, kumbukeni, Mataifa walikuwa wanajiandaa kuteketezwa, kama tu ilivyo sasa. Ulimwengu wa Mataifa unafaa kuangamizwa kwa moto. Tunajua hilo.

¹³⁶ Sasa angalia ishara kuu. Mungu alishuka chini katika umbo la Mtu na akafanya ishara, huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, na kuuliza mahali alipokuwa Sara. Ndipo Ibrahimu akasema, “Yuko ndani ya hema nyuma Yako.”

¹³⁷ Na Yeye akasema, “Mimi nitakuzuru kulingana na wakati wa uhai.” Angalia hilo “Mimi,” unaona, “Mimi nitakuzuru.”

¹³⁸ Pia, tazama, Yeye hakumwita Abram. Siku chache tu kabla ya hapo, yeye alikuwa ni Abram. Lakini Mungu alibadilisha jina lake, katika Roho, akizungumza na yeye. Lakini huyu hapa Mungu katika mwili; alikuwa ndiyo kwanza ale nyama ya ndama ambaye Ibrahimu alimchinja, akinywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, na kula mkate. Wazia hilo. Mtu, mwenye mavazi yaliyojaa vumbi, miguu michafu, amina, Mungu!

Unasema, “Huyo hakuwa Mungu.”

¹³⁹ Ibrahimu alisema alikuwa, alisema Huyo alikuwa ni “Elohimu,” Yule ambaye aliumba mbingu na nchi, Yule anayejitosheleza kwa yote, Mungu katika umbo la mwanadamu. Amina.

¹⁴⁰ Na Yeye alifanya ishara kwa Ibrahimu, kumfanya ajue hilo, kwamba ulimwengu wa Mataifa ulikuwa kwenye mwisho. Na Yeye alikuwa ni huo Uzao mkuu. Akasema, “Yu wapi Sara?”

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

Akasema, “Nitakuzuru kulingana na wakati wa uhai.”

¹⁴¹ Naye Sara akafanya jambo fulani. Kwa namna fulani alicheka. Akasema, “Kwa nini Sara akacheka, akisema, ‘Mambo haya hayawezekani?’” Alitambua mawazo yaliyokuwa niani mwa Sara, katika hema nyuma Yake. Ndipo akajua huyo alikuwa ni Mungu.

¹⁴² Sasa tazama. Yesu, wakati Yeye alipokuja duniani, Yeye alikuwa ni ule Uzao mkuu. Basi, wakati Yeye alipokuja, aliwatangazia watu jambo lile lile. Je! hiyo ni kweli? Sasa, akijua kwamba wakati huu wa mwisho ulikuwa unakuja, kisha kasema, “Mambo nifanyayo nanyi mtafanya vivyo hivyo, kwa sababu Mungu alisema ninaenda kuwapa ishara ya Milele, isiyo na mwisho.” Amina. Hiyo hapo ishara kuu.

¹⁴³ Tazama mkondo wa kanisa. Limekuja kupitia Luther, Wesley, Pentekoste, madhehebu. Tumekuwa na funuo na namna zingine zote za mambo. Tulikuwa na kunena kwa

lugha. Tumekuwa na karama za uponyaji. Tuna kila kitu kikidhihirishwa.

¹⁴⁴ Lakini, tazama, moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho, kabla ya kuteketeza na kuangamiza, ishara kuu inaonekana kiajabu, moja kwa moja jukwaani tena mbele zetu, amina, Mungu Mwenyewe. Si mwanadamu, bali Mungu akidhihirishwa; ishara kuu, ishara isiyo na mwisho, ishara ya Milele, ishara kuu, Mungu akidhihirishwa katika mwili! Ishara ile ile ambayo Mwana Wake alifanya, Mwana Wake mkuu aliahidi iyo hiyo kwenye wakati wa mwisho, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati wa Kuja kwa Mwana wa Adamu.” Ishara kuu itarudi.

¹⁴⁵ Tumekuwa na vitu hivi vingine vyote, njia ya Uzao wa kifalme wa Ibrahimu imepitia njia ile ile ambayo Ibrahimu alipitia.

¹⁴⁶ Lakini kabla tu ya kuangamizwa kwa ulimwengu, ishara kuu lazima ijitokeze tena, ishara ya ufufuo isiyo na mwisho, ya Milele inayohibitisha kwamba Uzao mteule usingeweza kuuawa kama Danieli na kama manabii wengine wote walivyokuwa. Kaburi halikuweza kumshikilia. Kwa sababu Yeye... Wale wengine walishinda malango ya adui, kama vile moto, na simba, na—na upanga, na kadhalika. Walishinda hiyo. Bali huyu Uzao wa kifalme alishinda kifo, kuzimu, na kaburi. Hakuna kitu kingaliweza kumshikilia. Kwa nini? Yeye ni ishara kuu ya milele! Ishara kuu ni kitu gani? Kufufuka kwa Yesu Kristo, baada ya kuwa amekufa kwa miaka elfu mbili, angali anasimama miongoni mwetu, kama Yeye alivyofanya wakati ule, akijidhihirisha Mwenyewe katika Kanisa Lake, katika mwili wa binadamu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina.

¹⁴⁷ “Bikira atachukua mimba. Na kuanzia wakati huo, Mungu na mwanadamu watakuwa mmoja, wameunganika pamoja,” ishara ya Milele, isiyo na mwisho, ishara kuu.

Anaishi, anaishi,
Kristo Yesu anaishi leo hii!
Huenda ukaniuliza jinsi ninavyojua Yeye
anaishi?
Yeye anaishi ndani ya moyo wangu.

¹⁴⁸ Ninamwona Yeye miongoni mwetu. Wote wa Uzao Wake mteule wataiona. Naam, bwana.

¹⁴⁹ Wateule katika siku Yake waliiona. Waliochaguliwa kimbele walipata kuiona. Katikati ya kutokuamini, bado waliiamini. Waliketi moja kwa moja miongoni mwa wasioamini na bado waliikiri hadharani, “Naam, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.” Loo, jamani!

¹⁵⁰ Moja kwa moja miongoni mwa maelfu ya wasioamini, mtu mmoja, jina lake Simoni Petro, alitokea. Ndipo Yeye akasema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yusufu.” Hiyo ilikuwa

ni kitu gani? Ile ishara kuu. Huyu hapo alikuwa ni Nabii amesimama hapo, hiyo hapo ilikuwa ishara kuu, naye Simoni Petro akaikubali haijalishi kile yeyote alichosema. Maskini jitu kubwa lenye nguvu likafanyika mwana-kondoo mnyenyekevu mbele za Mungu.

¹⁵¹ Tazama, kulikuwa na Nathanaeli, mwalimu, msomi kwelikweli, aliyemwamini Mungu. Ndipo Filipo akaenda huko na kumleta kutoka kwenye m—mji wake, akamleta. Alipokuja mahali Yesu alipokuwa amesimama, Yesu alisema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake.”

¹⁵² Akasema, “Rabi, ulinijua lini? Hili linashangaza. Nimewasikia babu wa babu wa babu wa babu zangu wakizungumza kuhusu *Fulani* na *Fulani*, huko nyuma. Sijawahi kusikia hilo katika ninii yangu . . . Wewe ulinijua?”

¹⁵³ Yesu akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Ishara kuu! Amina. Makuhani na marabi walikuwa wameisha. Hiyo hapo ilikuwa ishara kuu ya Mungu ya Milele. Naam.

¹⁵⁴ Ilimbidi kupitia Samaria. Kumbukeni, zipo jamii tatu za watu; watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Aliwapitia Wasamaria. Akatokea maskini mwanamke, kisimani, kuteka maji. Yesu, mara tu alipozungumza na mwanamke huyo, kasema, “Niletee maji ninywe.”

¹⁵⁵ Mwanamke huyo akasema, “Huna kitu cha kuchotea,” na kadhalika. Ndipo mazungumzo yakaendelea. Walizungumza kuhusu shida ya jamii, na kadhalika.

¹⁵⁶ Baada ya kitambo, Yeye akamwambia mwanamke huyo, “Nenda kamwite mume wako na mje hapa.”

¹⁵⁷ Sasa mwanamke huyo akasema, (“Mtu huyu anajaribu kujifanya mwerevu kwangu,”) unaona, “Mimi sina mume.”

¹⁵⁸ Kasema, “Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako.” Ishara kuu!

¹⁵⁹ Msikilize, “Bwana, naona kuwa Wewe ni Nabii,” ishara kuu, dhihirisho la Neno kwa ajili ya siku hiyo. Tazama. “Wewe ni Nabii, lakini sioni katika Biblia ambapo nabii yeyote anapaswa kuwa kwenye wakati huu. Bali tunatazamia Masihi, na, wakati Yeye akija, Yeye atadhihirisha Neno la Mungu lililoahidiwa. Huyu atakuwa Ndiye.”

¹⁶⁰ Maskini mwanamke huyo mdogo alijua mengi kumhusu Mungu kuliko nusu ya wahubiri wa siku hiyo, katika hali hiyo. Kwa nini? Alikusudiwa jambo hilo kimbele. Wakati Nuru hiyo ilipoiangazia, mbegu hiyo ikawa Hai. Huwezi kuificha. La.

¹⁶¹ Mwangalie Nathanaeli, hakujali—hakujali ni nani aliyesimama pale. Alisimama moja kwa moja mbele ya kuhani wake na wote, kasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli tunayemtazamia.” Aliiona ishara kuu.

¹⁶² Maskini mwanamke huyu, katikati ya masumbuko yote aliyokuwamo, alikimbia kupitia mjini, na akasema, “Njoni mwone Mtu aliyeniambia yale niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hicho si ndicho tunachotazamia?” Ishara kuu!

¹⁶³ Sasa, kumbukeni, Mataifa hawakuipokea wakati huo, lakini lazima waipokee maana Mungu hawezi kubadilisha mwendeleo Wake. Inambidi kufanya hivyo. Kumbukeni, Yeye aliahidi hilo. Alisema Yeye angefanya hivyo. Aliahidi Yeye angefanya hivyo. Na katika siku za mwisho, Yeye angefanya hivyo. Yesu alisema hivyo, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu.” Tumeahidiwa, katika siku za mwisho, kulingana na Malaki 4, kwamba mtu fulani atainuka katika siku za mwisho ambaye atajaribu kurudisha, na kutikisa na kuondoa ubaridi wote na mapokeo yao yote, na kadhalika, “na kurejesha Imani ya watu kwa baba wa kimitume tena, kwenye Neno la asili.” Naam.

Unasema, “Huyo alikuwa—huyo alikuwa Eliya katika Yohana.” Loo, la, siyo.

¹⁶⁴ Eliya katika wakati wa Yohana alikuwa Malaki 3, “Ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.”

¹⁶⁵ Kwa sababu, mara tu baada ya unabii *huu* kutokea, ulimwengu wote uliteketezwa. Miaka elfu mbili imepita, na ulimwengu haukiteketezwa. “Nao wenye haki wanatembea juu ya mavumbi ya—ya majivu ya waovu.”

¹⁶⁶ Ndugu, dada, tunaishi katika siku za maduka makubwa, jeti kuu, barabara kuu, jamii kuu, kila kitu kingine kikuu. Na kuna ishara kuu! Tumekuwa na ishara ya dini. Tumekuwa na ishara ya miamsho. Tumekuwa na ishara ya kuunganika. Tumekuwa na ishara ya kunena kwa lugha. Tumekuwa na ishara ya kuwaponya wagonjwa. Tumekuwa na ishara hizi zote.

¹⁶⁷ Bali, hata hivyo, tunakuta katika Biblia kwamba, ishara ya mwisho kabla ya Mwana aliyeahidiwa kuwasili, ilikuwa ni ishara kuu. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa wakati huo; kabla ya Mwana aliyeahidiwa kuwasili tena, hiyo ishara kuu itarudi duniani tena.” Ninawatangazieni, usiku wa leo, katika Jina la Yesu Kristo, iko duniani sasa. Si hiyo tu, bali ipo papa hapa miongoni mwetu usiku wa leo. Roho Mtakatifu, ishara kuu ya Mungu, Yesu Kristo aliyefufuka, Huyo hawezi kushindwa. Ni ishara ya Milele. Kamwe haiwezi kubadilishwa. “Mbingu na nchi zitapita, bali Hiyo haitabadilika kamwe.” Ni ishara ya Milele, isiyo na mwisho, Mungu akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu. Mungu alijitambulisha Mwenyewe katika mwili wa binadamu.

¹⁶⁸ Je! unaamini hiyo kuwa ni Kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kwa moyo wako wote, unaamini hilo? [“Amina.”] Usijifungie mwenyewe kama kasa kwenye gamba. Iwapo kuna kasa yeyote ndani yako, ondolea gamba mbali.

Acha Roho Mtakatifu aingie ndani. Usijifungie mwenyewe kwenye kanuni fulani ya imani au dhehebu. Ndugu, dada, saa imewadia. Ninaamini kwamba Mungu amefanya mengi kama Yeye anavyoenda kufanya. Jambo linalofuata ni tendo la kanisa ama vinginevyo tunaenda kupotea.

¹⁶⁹ Ninauliza tu mtu yeyote abishe hilo kuwa hivyo. Nimeuliza kote na kote ulimwenguni, na si hata wakati mmoja ambapo kila mtu, yeyote amejaribu hilo kamwe. Wanajua vyema. Wanajua vyema, kwa sababu ni Neno, na Mungu huthibitisha Hilo ni Neno Lake. Basi kwa nini msilikubali? Amina. Kama ni wakati, usiliahirishe muda mrefu kupita kiasi.

¹⁷⁰ Watu wengi walitaka kumkubali Yesu. Walidhania wangefanya hivyo, “katika wakati mwingine unaofaa,” mmoja alisema. Wanataka kumpokea Kristo, lakini wanaliahirisha muda mrefu kupita kiasi. Baadhi yao walijaribu kumwondoa Yeye kwenye mikono yao, na kujaribu kuliondolea mbali kwa kuliosha na maji, kupitisha lawama kwa mtu mwingine, lakini ilienda kinyume na matarajio.

¹⁷¹ Liko mikononi mwako, usiku wa leo, limerushwa moja kwa moja mkononi mwako tena! Waebrania 13:8, bila kujali ni Mabaraza mangapi ya Makanisa tuliyo nayo, angali anabaki kama “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” “Kazi nizifanyazo!” Ikiwa—ikiwa Uhai Wake uko ndani yako, utadhihirisha Yesu Kristo. Amina.

¹⁷² Sasa nyinyi nyote hamwezi kuwa huyo, lakini mnaweza kuwa sehemu yake, kwa imani yenu.

¹⁷³ Wote hawangeweza kuwa Yesu, wakati walipokuwa duniani, lakini wangeweza kumwamini Yeye na kuukubali ujumbe. Kulikuwa na Musa mmoja, Eliya mmoja, Nuhu mmoja, kote chini, daima imekuwa hivyo, lakini wengine wote wangeweza kuukubali. Na wao hawangekuwa na huduma yoyote isipokuwa kulikuwa na mtu fulani kuamini hiyo. Yesu hangekuwa na huduma yoyote isipokuwa mtu fulani aliamini. Paulo hangekuwa na huduma yoyote isipokuwa mtu fulani aliamini.

¹⁷⁴ Roho Mtakatifu hana huduma yoyote kwa Neno, leo hii, isipokuwa mtu fulani yuko tayari kuondokea kanuni yao ya imani na kurudi kwenye Neno tena, haijalishi jinsi lilivyo jema hapa na jinsi lilivyo halisi hapa. Lipo hapa sasa. Ninajua lipo hapa. Ninalihisi. Ninajua lipo hapa. Neno linasema lipo hapa. “Popote wawili au watatu wamekutanika katika Jina Langu, niko miongoni mwao.” Na kwa kweli ninaamini kwamba Yeye yupo hapa, “yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹⁷⁵ Loo, laiti ningaliweza kuifanya maskani hii ndogo... ninawapenda. Na siamini yupo mtu duniani ambaye ningeweza kusema nilimpenda zaidi ya Jack Moore, na, hiyo ni kweli, Young Brown, na Lyle, na watu hawa hapa. Nilisoma makala leo hii, ambayo Anna Jean aliandika, nilikuwa ninaenda kuomba

idhini yake kuichapisha tena, kwa mambo mazuri wanayoweza kusema. Pia—pia, tazama, bali usipoamka, upesi, itakuwa imechelewa mno. Maskani ya Life, mimi ni sehemu yenu, na hiyo ndiyo sababu ninapiga makelele. Mwaka baada ya mwaka, ninaona inakuwa baridi. Huenda msitambue hilo, mnaishi moja kwa moja ndani yake, lakini dumuni katika huduma na halafu mrudi mkiwa na kumbukumbu za mwaka uliopita. Si niliwaambia kwamba huko nje katika hema lile dogo, usiku mmoja, “Tangu saa hii na kuendelea”? Ningesema nini kuhusu Shreveport wakati mwanamke yule alinipa ile makala chafu wakati ule?

¹⁷⁶ Mnakumbuka kile nilichosema wakati ule kuhusu Marekani, miaka mitatu au minne iliyopita, mitano, halafu kikaenea katika magazeti yote? Nilisema, “Mwaka huu Marekani itakubali Injili ama hawataikubali.” Wameikataa tangu wakati huo. Na kamwe hakutakuwa na u—uamsho mkubwa Marekani tena namna hiyo. Kama mnaniamini kuwa nabii, kumbukeni kwamba hilo ni Neno la Bwana. Angalieni tu na mwone kama haifi. Makanisa yanakufa. Yananyauka. Na hiyo inaniua, ndani yangu, kujua hilo, wanaume na wanawake ninaowapenda kuliko ninavyopenda maisha yangu mwenyewe, ambao nimewapa maisha yangu.

¹⁷⁷ Nimekuja miongoni mwenu kama ndugu yenu, si Mungu wenu; ndugu yenu, si adui yenu; ndugu yenu! Nimewaambia Kweli, na Mungu ameonyesha hivyo. Pamoja na kila neno nililohubiri, Yeye amelionyesha kuwa . . . Kweli hasa. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi ni kwa nini usikubali Hilo, ndugu, dada? Katika upendo wa Yesu Kristo, mbona usikubali Hilo? Kama utaamini tu hilo kuwa Kweli, ukubali tu Hilo kuwa Kweli, hayo ndiyo yote ninayokuomba ufanye.

¹⁷⁸ Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu. Ninaenda kukomea hapo katika huo muhtasari papo hapo. Nilisema nilikuwa ninaenda kufanya wito wa madhabahuni, na kumwacha Billy Paul asambaze kadi za maombi. Hatukuwa na kadi zozote za maombi, usiku wa leo, kulikuwa kumechelewa sana kuzisambaza. Ni—nilisahau ahadi yangu. Nitakuwa naye hapa kesho usiku, yapata saa kumi na mbili. Hatuhitaji kadi za maombi, hata hivyo. Daima nimejaribu kuwaondoa kwenye desturi hiyo, daima ya kuwekea mikono kama Wayahudi walivyofanya. Yairo alisema, “Njoo ukaweke mikono Yako juu ya binti yangu naye ataishi.” Mrumi alisema, “Nena tu neno,” hiyo ilikuwa ndiyo njia ya Mataifa ya kuliadini.

¹⁷⁹ Kama nimewaambia Kweli, sasa sikilizeni changamoto hii; kama nimewaambia Kweli, basi inanibidi kusimama hapa kwenye jukwaa hili mbele zenu na kuwaambia hili. Na inafaidi nini kuwaambia, kama Mungu hayuko ndani yake? Na kama ni Kweli ya Mungu, Yeye—Yeye anawajibika kuunga Hiyo mkono. Inambidi kuiunga Hiyo mkono. Yeye aliahidi angefanya hivyo.

¹⁸⁰ Lakini je! tu—tunaenda kuketi kama wasiojali? Je! Roho ame... Je! ni “Ikabodi” juu ya Maskani ya Life? Je! hiyo imeandikwa kwenye maskani? Hivi hiyo imeandikwa kwenye makanisa ambayo nimekuwa nikitembelea kote nchini? Je! ni giza sana na nzito sasa hata yule “mmoja *hapa* na mmoja *pale*; mmoja kondeni, ‘Nitamchukua mmoja,’ na labda mmoja upande ule mwingine wa ulimwengu, na, ‘Nitachukua mmoja’”? “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo nafsi nane ziliokolewa kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana,” je! tumefikia mahali hapo?

¹⁸¹ Je! huduma ya Yesu Kristo, katika siku hii, imefananisha siku ile ambayo Yeye alikuwa hapa wakati alipohubiri mara ya kwanza? Wakati Yeye alipokuwa Nabii kijana Mgalilaya, kila mtu alimtaka Yeye kanisani mwao, wakati alipowaponya wagonjwa, na kila kitu. Lakini wakati Yeye alipoanza kutabiri na kuwakemea, na kuwaita “kundi la nyoka,” papo hapo Yeye alianza kufifia, na hatimaye ikaelekeza kwenye kusulubiwa Kwake, kuuawa.

¹⁸² Lakini, kumbuka, Yeye alikuwa na huduma nyingine, Yeye aliwahubiria waliopotea na kuhukumiwa Milele, ambao hawakutubu katika siku walizokuwa na nafasi ya kutubu. Je! huduma hiyo itarudi namna hiyo, kwamba huduma itaendelea kuwaendea watu waliopotea na kuhukumiwa, ambapo hapana rehema ya kupatikana kwa ajili yao? Wazia hilo, vipi kama ingeweza...

¹⁸³ Unasema, “Ni hivyo, Ndugu Branham?” Sijui. Huenda kumechelewa kuliko tunavyofikiria.

¹⁸⁴ Ukiona kivuli cha kitu chochote, unajua kile kitakachokuwa kikiwa halisi. Ulinua mikono yako, na kuona vidole vinne, vidole vitano, chochote mkono wako utakachokuwa wakati kivuli kitakapofanyika kitu halisi, hicho ndicho ulicho katika kivuli.

¹⁸⁵ Aminini, enyi marafiki. Loo, Mungu awasaidie! Jamani, ni mara ngapi... Mmeninunulia suti za mavazi. Ninazo, kule nje sasa, zawadi, katoni za peremende, ndoo za shira. Hata mmeipa, fa—familia yangu, taalo; watoto wangu, nguo. Mmenilisha. Mmefanya kila kitu mlichoweza kufanya. Na sasa hebu niwafanyie jambo fulani. Hebu—hebu—hebu na tu...

¹⁸⁶ Loo, laiti Mungu angaliweza tu kuingilia, kwa njia fulani, sasa hivi! Kweni mlipo kwenye orofa ya juu, orofa ya chini, popote mlipo, kwenye roshani, Mungu asipounga mkono kile ninachosema, basi nimesema uongo. Lakini kama Yeye anakiunga mkono! Ninajua mmeona uigaji mwingi wa kimwili, lakini huo unapaswa kufanya kitu halisi kuangaza bora zaidi kweni. Iweni na imani, na mwamini.

¹⁸⁷ Bila shaka, hakuna kadi ya maombi jengoni. Kama ipo, inua mkono wako, yeyote aliye na kadi ya maombi kutoka kwenye

mkutano huu. Unaona, hakuna hata moja. Lakini wapo watu wagonjwa wanaoketi hapa. Na kama Roho Mtakatifu, papa hapa kwenye jukwaa hili, atafunua na kupitia kwenye wasikilizaji hawa na kuzunguka kupitia hapa kwenu enyi watu. . .

¹⁸⁸ Angalia kile Biblia ilichosema. Ni nini ishara kuu? Ni Neno lililodhihirishwa katika kila wakati. Hiyo ni kweli? Vema, ni kwa nini hawakuweza kumwamini Yesu? Wakati, Waebrania 4 ilisema kwamba, “Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, likipasua.” Hiyo ni wakati Hilo likihubiriwa katika nguvu Zake, Hilo hukata kulia na kushoto, lina ncha mbili, hukata pande zote. Ni kitu gani? “Hukata hata kwenye mafuta ya mfupa.” Na hufanya nini kingine? “Hutambua mawazo yaliyoko moyoni.”

¹⁸⁹ Yesu akisimama pale, nao unabii Wake ukiwakata hao watu wa kidini vipandevipande, na kuwaita “kundi la mashetani,” juu ya watu; na kulilia msamaha wao wakati walipomsulubisha.

¹⁹⁰ Kama Ndugu Jack alivyosema wakati mmoja, alitoa tamshi, “Watoto Wake Mwenyewe wakililia Damu Yake.” Hiyo ni kweli.

¹⁹¹ Alikuwa akijaribu kuwaokoa kutoka kwenye jehanamu la ibilisi. Na walipoona utambuzi huo ukiendelea, kwa nini hawakujua, kujua kwamba hiyo ilikuwa ni ishara kuu ya Mungu? Sababu ile ile kanisa halijui leo hii. Lakini popote Nuru hiyo inapoangazia ile mbegu iliyokusudiwa, itakuwa Hai. Ndiyo, hasa, huwezi kuizuia.

¹⁹² Jua la mwanga huko juu, j-u-a, linadhibiti uhai wote wa mimea. Mbegu ikiwa hapo na jua liiangazie, itachipuka kuwa hai. Naam, bwana.

¹⁹³ Naye M-w-a-n-a wa Mungu ndiye mdhibiti wa Uzima wote wa Milele. Na iwapo una mbegu ya Uzima ndani yako, ndugu, wakati huyo M-w-a-n-a akiangaza hapo na kukuonyesha kile aliche Yeye, inachipuka kuwa Hai. Hakuna njia ya kuizuia na huo.

¹⁹⁴ Wewe amini sasa. Amini tu. Kuwa na imani katika Mungu wakati tukiomba kwa kicho.

¹⁹⁵ Baba wa Mbinguni, hizi hapa mbele zangu zimewekwa lundo la vitambaa, lesa. Ee Mungu, kila mtu anakuamini Wewe kama mponyaji. Hakika. Watu wote wa full-Gospel wanakuamini Wewe hivyo. Wewe ni mponyaji, na Wewe ni mwenye fadhili sana na mwenye rehema kwao. Moja kwa moja kwenye saa za kusulubiwa Kwako, Wewe ungali uliponya, ukarudisha sikio la a—akida wa Kirumi tena, ambalo Simoni alikata kwa upanga wake. Adui aliyekuja kukushika Wewe, Wewe ungali ulikuwa mwema na mwenye rehema kuponya. Ungali unafanya jambo lile lile.

¹⁹⁶ Bali, Bwana, je! macho ya watu yanaweza kufumbuka na waone kwamba kile tunachojaribu kuwaambia, kwamba ni—ni

wakati wa mwisho! Ninaomba, Mungu, ninaomba katika Jina la Yesu, jalia litendeke usiku wa leo, Bwana. Jalia Maskani ya Life ichukue jina lake usiku wa leo, Uzima, Uzima wa Milele. Kundi lote lililoko chini ya bendera zake hapa usiku wa leo, jalia Uzima uje, kwa wingi.

¹⁹⁷ Baada ya Neno kuwekwa hapa nje, dhahiri tu kama Hilo linavyoweza kuwa, ahadi ya siku hii, Wewe uliahidi Hiyo katika siku hii. Tunajua hilo, Bwana.

¹⁹⁸ Na sisi ni watoto wa Ibrahimu, tumekuja, kuteremka kupitia kama Ibrahimu alivyofanya. Kutoka kuvuka; kukiri. Kuja huku katika nchi ya kigeni; tulifanya hilo, tumekuwa na maono na funuo, na kila kitu, cha Mungu. Jinsi Yeye alivyotuzungumzia na kutuponya, na kufanya mambo yale yale ambayo Yeye alimfanyia Ibrahimu! Bali katika wakati wa mwisho, kabla tu ya Mwana aliyeahidiwa, ndipo Mungu akaonyesha kile wakati wa mwisho ungekuwa, kwa ishara kuu.

¹⁹⁹ Ndipo basi Mbegu kuu, Yesu Kristo, Mbegu ya imani, inashuka chini na kufanya jambo lile lile katika mwisho wa Wayahudi, kama walivyofanya kule katika mwisho ule.

²⁰⁰ Na sasa katika mwisho wa vitu vyote, Yeye aliahidi kuja tena. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na katika siku za Sodom." "Kazi nizifanyazo Mimi, nanyi pia mtazifanya." Kama Uhai Wake umo ndani yetu, Huo humwakisi Yeye. Unaakisi mjenzi, mtengenezaji wa bidhaa; kazi yake daima humwakisi yeye, mwenyewe. Na Mungu aliakisiwa katika Kristo, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi."

²⁰¹ Na sasa ninaomba, Mungu, kwamba Wewe utamponya kila mmoja wa hawa ambao ninawaombea kwa uaminifu. Waponye, Bwana. Tujalie hilo.

²⁰² Na sasa, mpendwa Baba wa Mbinguni, hapa nimesimama. Ninatambua si—siwezi kuwa hapa muda mrefu zaidi, na ninaona maisha yangu ya kimwili yakitoweka. Saidia, usiku wa leo, Bwana, mara hii moja. Mara moja zaidi, Bwana, jalia kwamba—kwamba watu watasahau yaliyopita sasa, na wakaze mwendo kuelekea mede ya wito wa juu. Tujalie, Bwana.

²⁰³ Ninaenda kukuomba Wewe kufanya jambo fulani ambalo linaenda kuwa ni jambo gumu, Baba. Ninatambua hilo. Bali ninaenda kukuomba Wewe kumwachilia Yesu aje ndani yetu. Pia, Baba, ili tu kunitia upako, kusingelifaidi sana kusanyiko hili isipokuwa Wewe uwapake mafuta, pia. Sisi—sisi ni kitu kimoja, pamoja. Na uwapake na imani, kwamba mtu fulani hapa . . . Kwa hakika yupo mtu fulani aliye na imani ya kutosha kufanya hilo, kama yule mwanamke aliyeligusa vazi Lake. "Na Yeye ndiye Kuhani Mkuu hivi sasa awezaye kuguswa na hisia ya udhaifu wetu," kuonyesha kwamba Yeye angali ni ile ishara kuu, Mungu ndani ya mwanadamu, Mungu akifanya kazi kupitia mwanadamu, wasioelimika na wale watakaojisahau wenyewe,

na kumwacha tu Roho afanye kazi kupitia wao. Wapo maskini wanawake wanaoketi hapa ndani, wanaoteseka, labda, na kitu kile kile ambacho mwanamke yule alikuwa nacho. Wapo kina Simoni wameketi hapa ndani, usiku wa leo, Bwana, wa—wana wa kina Yona, kama ilivyokuwa. Wameketi hapa. Saidia sasa, Bwana, kwamba watu waweze kujua.

²⁰⁴ Na ujibu maombi yangu vile mimi. . . Si kupitia msisimko; ninajua nina msisimko, bali mimi kabisa. . . Ninasumbuka, Bwana, ninapoonamambo yakienda jinsi yanavyoenda. I—inanichosha kwamba ninii. . . Hebu watu warudi kwenye Neno, na kusahau vitu hivi vyote maridadi vya wakati huu, maoni yanayopendwa na watu ya ulimwenguni; warudi kwenye Neno, Neno lililodhihirishwa kwa wakati sasa ambao tunaishi. Tujalie, Bwana.

²⁰⁵ Na huku tumeinamisha vichwa vyetu, ninataka kila mmoja wenu aombe, kwa—kwa urahisi tu. Usininii. . . Endelee tu kuinamisha vichwa vyenu na mwendelee tu kuomba, useme, “Bwana, nisaidie sasa.”

²⁰⁶ Na uwe na kitu niani mwako ambacho unataka kuombea. Na kama Bwana Yesu angali hai, basi kwa hakika, enyi rafiki, hiyo itakuwa ndiyo ishara kuu. Na watu wengine wamesema, “Loo, hapana shaka hilo linaweza kufanywa, Ndugu Branham anayo karama kubwa ya Bwana. Nami ninaamini, wakati akiwa chini ya upako, yeye ni nabii wa Bwana, bali msisikilize Fundisho lake.” Sasa mtu yeyote angefanya hilo, angesema hilo, na anapaswa kuwa ni msomi? Wakati, hiyo ndiyo ishara yenyewe kwamba Fundisho ni sahihi, kulingana na Biblia.

²⁰⁷ Na iwapo wewe ni mwenye dhambi, kidimbwi kinangojea pale. Ikiwa hujawahi kubatizwa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zako, kidimbwi kinangojea. Iwapo hujapokea Roho Mtakatifu bado, lazima uwe na ile Ishara juu yako la sivyo hutapita kwenye Lango. Lazima uwe ni Uhai wa Kristo ndani yako.

²⁰⁸ Sasa wewe omba na umwulize Mungu akusaidie, wakati tukiomba sasa. Nanyi dada kwenye vyo—vyombo hapo, “Amini Tu.”

²⁰⁹ Wazia tu, akishuka mlimani alikuja Yesu. Katika mawazo yako tu ya akilini, mwone Yeye akitembea kuja mlangoni, na kutembea kuja hapa chini na kusimama katika mimbara hapa, na kusema, “Watoto.” Liwazie tu niani mwako sasa.

²¹⁰ Na kila mtu kuwa na kicho kabisa, na uwe mtulivu kabisa na uombe. Kila mahali, endelea tu kuomba, ukisema, “Bwana Yesu, nirehemu. Bwana, ninaamini.”

²¹¹ Baba, Mungu, wamenyamaza sasa. Wakati huu wenye kicho, ninaamini Wewe upo hapa. Ninaamini hilo, ile Nguzo kuu ya Moto iliyowaongoza Israeli kupitia nyikani, iliyodhihirishwa katika mwili. Yeye alisema alikuwa. “Kabla Ibrahimu

asijakuwako, MIMI NIKO. Ninatoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.”

²¹² Baada ya kifo Chake, kuzikwa, kufufuka, na kupaa juu; Paulo alikutana na Yeye barabarani, akishuka kwenda Dameski. Nuru kuu ilimtwanga ikamwangusha chini. Huyu Mwebrania asingemwita Yeye “Bwana” kama hakujua hiyo ilikuwa ni Nguzo ile ile ya Moto. “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

²¹³ Na hapa Wewe upo usiku wa leo, pamoja nasi, Uhai ule ule ndani yetu. Ninakushukuru Wewe kwa Huo, Baba. Sasa jalia ijulikane kwamba nimesema Kweli. Na hiyo . . . Yule bikira kuchukua mimba, kuleta mwanadamu na Mungu pamoja, ndiyo ishara ile ile iliyo miongoni mwetu usiku wa leo kwenye mwisho wa wakati, ishara kuu. Jalia iwe mara nyingine tena, Baba. Ninaomba kupitia Jina la Yesu Kristo.

Sasa endeleeni tu kuomba.

²¹⁴ Sasa ninachukua kila roho hapa ndani chini ya udhibiti wangu, katika Jina la Yesu Kristo. Sasa kama unataka kuomba, endelea kuomba; kama unataka kuangalia juu, fanya chochote utakacho sasa. Endelea kushikilia ushuhuda wako. Endelea kushikilia imani yako, kama unaomba.

²¹⁵ Ninaona, nje mbele zangu sasa, katika marefu haya ya katikati hapa, maskini mama, mwanamke, ameketi papa hapa nyuma, ambaye ndio kwanza ainue kichwa chake; katika marefu haya ya katikati, mbali huko upande wa nyuma. Yeye anaogua tatizo la mgongo. Naam. Je! unaamini kwamba Mungu ataponya mgongo wako? Unaamini? Vema. Hilo ndilo ulilokuwa unaombea. Je! hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Nyote wawili mmeponywa. Mama huyo moja kwa moja karibu na yeye alikuwa na shida ya mgongo, pia, maana aliinua mkono wake. Niliiona ikitoka kwake kwenda kwake. Sasa, siwajui, siyoy, si hata mmoja wenu? Lakini hilo ndilo lililokuwa sahihi. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Sasa je! hiyo ndiyo ishara kuu?

²¹⁶ Hapa, moja kwa moja nyuma katika marefu *haya*, kwenye ninii wangu. . . upande *huu* moja kwa moja karibu huko nyuma, yupo maskini mwanamke asiyeweza hata kumeza, karibu. Kuna jambo lililo kasoro na yeye—na yeye—kumeza kwake. Ni vigumu kwake kumeza. Lakini anaamini. Anatoka nje ya mji. Je! utaamini, dada, kwamba utakuwa kwamba unaweza kumeza? Utakubali uponyaji wako? Inua mkono wako kama utakubali. . . Vema, sasa unaweza kuponywa. Sasa, ikiwa kwamba, kama mimi ni mgeni kwako, punga mkono wako namna *hiyo*. Hiyo ni kweli, unaona. Lakini, hilo ndilo, alikuwa ameketi papo hapo basi akijaribu kumeza. Sasa, meza sasa na unaweza kumeza vizuri. Uone kama hiyo ni kweli.

217 Je! mnaamini kwamba Malaika wa Bwana yupo hapa? Je! mnaamini hiyo, ishara kuu? Hao watu, kote katika jengo. Mtu fulani hapa juu, karibu. Nitageuza mgongo wangu, ili kuwafanya tu mjue, katika kila hali, kwamba Huyu ni Bwana Yesu. Nitageuza mgongo wangu. Na mtu fulani aombe, amini. Kama unafikiria ninakuangalia, ili kama kusoma mawazo yako, ama jambo fulani, wewe amini tu. Kama Yeye angeweza kujua kile ambacho Sara alikuwa akiombea, ama kile alichokuwa akifanya katika hema nyuma Yake, maana Mungu alidhihirishwa katika mwili wa kiumbe, mwanadamu aliyekuwa anakula, anakunywa, ishara! Nimewaambia ilikuwa ni ishara kuu.

218 Naam, huyu hapa mwanamume anayekuja mbele zangu sasa. Amesimama moja kwa moja nyuma yangu. Yuko papa *hapa* nyuma. Yeye anakuwa kipofu. Jina lake ni Maclusky. Kama ataamini kwa moyo wake wote, Mungu atamponya. Simama. Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu. Amini, bwana.

219 Vipi kuhusu huku upande *huu*, je! mtaamini hapa? Unaamini kwa moyo wako wote? Wewe omba.

220 Ninamwona mwanamke, na yeye anaugua kitu fulani. Anafikiri ni kifafa, kwa sababu yeye huzirai. Ametoka Kusini-mashariki, kutoka... Anatoka Florida. Na jina lake ni Bibi Kinney. Kama utaamini, Bibi Kinney, na kusimama kwa miguu yako, utaponywa vipindi hivyo vya kuzirai. Simama kwa miguu yako. Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa. Mwulize.

221 Je! mnaamini kwamba Yeye ndiye ishara kuu? Vipi kuhusu sehemu *hii*, mnaamini?

222 Mwanamke anayeugua, karibu kurukwa na akili, moja kwa moja upande *huu*. Jina lake ni Bibi Jones. Kama ataamini kwa moyo wake wote, anaweza kuponywa. Bibi Jones, kama utaamini, na kusimama kwa miguu yako na kuamini kwamba Yesu Kristo anakupa afya, unaweza kuwa na uponyaji wako. Yeye, mgeni kabisa kwangu mimi, sijawahi kumwona maishani mwangu. Mungu anajua hiyo ni kweli.

223 “Bikira atachukua mimba na atazaa Mwana, na Jina Lake litaitwa *Imanueli*, ambalo likitafsiriwa ni, ‘Mungu pamoja nasi,’” Mungu hapa ndani yetu, ishara kuu ya Mungu!

224 Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, tuko wakati wa mwisho. Kama Yeye yupo hapa, kwa nini usimkubali sasa? Mnaona jambo linalopaswa kutendeka? Mnaona linalopaswa kutukia? Kila mtu hivi sasa anapaswa kuponywa kikamilifu. Yupo Mtu, kipo Kitu fulani hapa kufanya hilo. Kila mtu anajua hilo.

225 Mungu Mbinguni anajua sijui hata mmoja wa watu hawa. Wao ni—wao ni wageni kabisa. Waulizeni mwone. Sijui chochote kuwahusu. Sijui wao ni kina nani, mahali wanakotoka, wala chochote.

²²⁶ Lakini kama mtachukua neno langu kwa hilo, kama hiyo ni kweli, nitasema sasa hivi, kwenu, Roho Mtakatifu anazunguka tu mahali hapa pote. Nuru hiyo imezunguka tu mahali hapa. Sasa kama Neno ni kweli, na Neno limedhihirishwa mbele zenu, shida ni nini hata hatulipokei Hilo? Ni nini kinachofuata, ndugu?

²²⁷ Uko katika shida, pia, kitu fulani kuhusu. . . Mbona, ni mke wako. [Mtu fulani anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Dakika moja tu mpaka nione ni kitu gani. Umeikiri, hebu na itoweke katika hilo.

Ninakusai kumwamini Mungu sasa hivi, ishara kuu!

²²⁸ Kitu pekee ni juacho kuhusu mvulana huyo, nilimsalimia kwa mkono. Siwezi kukuambia jina lake sasa. Lakini hasa hiyo ndiyo shida. Sijui hiyo. Nilikuwepo siku ile alipofunga ndoa, lakini jambo fulani limefanyika. Sitaki kulisema hapa.

²²⁹ Lakini, vema, hivi hamumwamini Mungu? Yeye alisema ishara hii kuu ingefanyika. Ni wangapi wanaotaka kumwona Yeye? Hebu tuone mkono wako, useme, “Mimi, nitamwamini.” Amina. Kwenye orofa ya chini, popote ulipo, juu kwenye roshani, kumbuka ishara kuu ya Mungu, Neno la ahadi, limedhihirishwa papa hapa leo hii mbele zenu, siku hii.

²³⁰ Yesu alisoma Maandiko, kisha akageuka na kusema, “Leo hii unabii huu umetimia miongoni mwenu.”

²³¹ Ninasema, katika Jina la Yesu Kristo, leo hii ishara ya wakati wa mwisho imedhihirishwa mbele zenu.

²³² Ni wangapi walio wagonjwa? Inueni mikono yenu. Katika Jina la Yesu Kristo, katika Uwepo Wake, kama unaweza kuamini kile ambacho umeona, kuwa ni Kweli na kinatoka kwa Mungu, ninakuomba katika Jina la Yesu Kristo, simama na ukubali Hicho basi, useme, “Nitakikubali. Nitakikubali, kitanitoshelezea. Ninaamini.” Sijali mahali ulipo. Hilo ni jema. Inueni mikono yenu sasa. Sasa mpeni tu Mungu sifa. [Mtu fulani anasema, “Leso?”—Mh.] Tayari nimeziombea.

²³³ Sasa msifuni tu Yeye, simameni hapo. Ishara kuu, ishara kuu moja—moja kwa moja miongoni mwenu, ishara kuu ya Mungu kwa ajili ya siku ya mwisho! Amina.

Mungu akubariki, ndugu.



ISHARA KUU SWA63-1129

(The Super Sign)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 29 Novemba, 1963, katika Maskani ya Life kule Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org